**MADA**

# MATUMIZI YA TAKRIRI NA SITIARI KATIKA *UTENZI WA RASI'LGHULI*

**NA**

**JUSTUS MAUNDU NDUMBU**

**C50/65902/2011**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA KISWAHILI.**

**OCTOBA, 2013**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine

_______________________________ _______________________________

Sahihi Tarehe

Justus Maundu Ndumbu

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi.

_______________________________ _______________________________

Sahihi Tarehe

Prof. Abdulaziz M.H

(Msimamizi)

_______________________________ _______________________________

Sahihi Tarehe

Prof. Kineene wa Mutiso

(Msimamizi)

## TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia kwanza kabisa bibi yangu mpendwa Mercy Mshai kwa kunisaidia kwa hali na mali wakati nilipokuwa ninasoma. Pia kwa kunipa moyo wa kuendelea na kazi yangu ya utafiti pamoja na kunipa utulivu wa moyo na akili. Pia watoto wangu William Ndumbu, Charles Ngewe, Janet Mbeke na Peris Sasara kwa kunivumilia sana nikiwa masomoni. Hata hivyo sitasahau kuwashukuru ndugu zangu Ben, Francis, Marehemu Charles, Daniel, Marehemu Beatrice, Agnes, Monicah, Nahum na Regina pamoja na mabibi na mabwana zao na watoto wao kwa kunisaidia kwa njia moja au nyingine katika masomo yangu ya awali Mungu awabariki wote.

# SHUKRANI

Kwa kweli kazi hii imekuwa na panda shuka nyingi sana lakini kwa usaidizi wa watu mbalimbali niliweza kuikamilisha. Kwanza ningependa kumshukuru muumba wangu Mungu aishiye milele, kwa kunipa siha njema na akili timamu, pamoja na hekima, ili kufanikisha malengo yangu ya kiusomi. Ni kupitia kwa nguvu na uwezo wake, ambapo nimeweza kuitimiza ndoto yangu, ya kupata shahada ya uzamili, katika somo la Kiswahili

Shukrani zingine nazitolea wasimamizi wangu; Prof. Abdulaziz M.H. na Prof. Kineene wa Mutiso kwa kunielekeza hatua kwa hatua, kunikosoa na kunirekebishia kazi yangu pamoja na kunivumulia. Ni kupitia kwa juhudi zao ambapo kazi yangu iliweza kukamilika na kuwa ya kutamanika. Shukrani za kipekee pia zimwendee Prof. Kineene kwa kunipatia *Utenzi wa Rasi'lGhuli,* kama si yeye singeupata

Shukrani zingine ziwaendee wahadhiri wangu wapenzi walionifunza. Prof.John Habwe, Prof.Kineene Wa Mutiso,Dkt. Zaja Omboga Dkt. Iribe Mwangi, Dkt.Evans Mbuthia, Dkt.Jefwa Mweri, Dkt, Mwenda Mbatiah na Bw. B. G. Mungania. Vilevile wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambao wengi pia walinifunza na kunisaidia kwa njia moja au nyingine. Mungu awabariki nyote na awape hekima na siku nyingi ili msaidie wengine kama mimi.

Ninawashukuru pia wasomi wezangu tulioshirikiana na kushauriana pamoja na kuhimizana na kuchukuliana mizigo. Sana sana sitasahau mahubiri na maombi tuliyokuwa tukianza nayo kila asubuhi. Wao ni Chacha, Makange, Onyonka, Owala,

Muriithi, Ombogi, Muniu, Ogutu, Keter, Meroline, Nguti, Njeri, Katutu, Suakei, Moraa, Grace, Rono, Florence, Lily, Rose, Salina, Juliet na Anjela. Asanteni kwa ushirikiano wenu. Ninawashukuru walimu wote wa Shule ya Upili ya Kamanzi pamoja na Shule ya Upili ya Mukimwani kwa ushirikiano wao. Mwisho ningependa kutoa shukrani za kipekee kwa mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Mukimwani Bw.Joshua Mbondo kwa ushauri wake na kunielewa kila nilipohitaji ruhusa ya kuhudhuria shughuli zangu za kimasomo. Wengine ni marafiki wangu wa dhati Bwana Joseph Ndunda kwa kunipa moyo na msaada niliohitaji pamoja na Joseph Ledemi Makange.

Sitasahau kumshukuru Sylvia Akendo kwa kujitolea kunipigia chapa kazi zangu zote za kiusomi pamoja na kupanga na kurekebisha makosa yaliyojitokeza. Barikiwa sana. Kwenu nyote ambao sikuwataja kwa majina na ambao mlinifaa kwa njia moja au nyingine, ninawashukuru sana na Mungu awamiminie baraka zisizo na kikomo.

## MUHTASARI


Utafiti huu unashughulikia matumizi ya takriri na sitiari katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli.*

Tasnifu hii ina sura tano, katika sura ya kwanza tumetanguliza kuhusu mada tuliyoshughulikia,usuli, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka, yalioandikiwa kuhusu mada hii, mbinu za utafiti na msingi wa nadharia ya utafiti.

Katika sura ya pili tumejadili tamathali za usemi,dhana ya fani, takriri, aina za takriri kama vile takriri irabu/vokali, takriri konsonanti, takriri neno/maneno na takriri silabi. Pia tumerejelea ufafanuzi wa sitiari kama tamathali ya usemi, aina za sitiari kama vile sitiari ya usuli, sitiari radidifu, sitiari ya kikaida, sitiari hisimseto na sitiari mseto.

Katika sura ya tatu tumeshughulikia kwa kina matumizi ya sitiari katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli.* Tumetoa mifano mahsusi ya aina za sitiari ambazo zilijitokeza kwa wingi. Pia tumependekeza beti kadhaa ambazo mbinu hii ya sitiari imetumiwa katika utenzi mzima.

Kama vile ilivyo sura ya tatu, katika sura ya nne tumejikita katika ufafanuzi wa takriri katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani. Tumechunguza aina za takriri na jinsi zilivyotumika katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli.* Tumetoa mifano kadha wa kadha kutoka kwa utenzi wenyewe na kupendekeza beti zaidi za kurejelewa.

Baadaye katika sura ya tano tumetathmini malengo ya utafiti pamoja na nadharia tete. Kulingana na maoni yetu, tulifanikiwa kutimiza malengo yetu, pamoja na kuthibitisha nadharia tete ambazo tulitoa mapendekezo ya yale ambayo yanahitajika kufanywa katika

*Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Yakiwemo uchunguzi wa kina katika vipengele kama, maudhui, dhamira, mandhari, toni, usimulizi na kadhalika.  Pia tulipendekeza matumizi ya nadharia zingine katika kuhakiki utenzi wenyewe.

## YALIYOMO

UNGAMO .......... iii

TABARUKU .......... iv

SHUKRANI .......... v

MUHTASARI .......... vii

YALIYOMO .......... ix

**SURA YA KWANZA .......... 1**

1.0 Utangulizi .......... 1

1.1 Usuli .......... 2

1.2 Tatizo la utafiti .......... 4

1.4 Sababu za kuchagua mada hii .......... 6

1.5 Upeo na mipaka .......... 7

1.6 Nadharia tete .......... 8

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii .......... 8

1.8 Mbinu za utafiti .......... 10

1.9 Msingi wa nadharia ya utafiti .......... 11

1.10 Hitimisho .......... 13

**SURA YA PILI: MAELEZO YA KIMSINGI YA DHANA YA TAKRIRI NA SITIARI .......... 14**

2.1.0 Utangulizi .......... 14

2.1.1 Dhana ya fani .......... 14

2.1.2 Tamathali za usemi .......... 15

2.1.3 Takriri .......... 16

2.1.4 Aina za Takriri ........ 17
2.1.5 Takriri Irabu/Vokali ........ 17
2.1.6 Takriri Konsonanti ........ 18
2.1.7 Takriri – Neno / Maneno ........ 18
2.1.8 Takriri Silabi ........ 19
2.1.9 Ufafanuzi wa sitari kama tamathali ya usemi ........ 19
2.1.10 Aina za Sitiari ........ 21
2.1.11 Sitiari kuu ........ 21
2.1.12 Sitiari Sahili ........ 21
2.1.13 Sitiari Chakavu ........ 22
2.1.14 Sitiari ya usuli ........ 22
2.1.15 Sitiari radidifu ........ 23
2.1.16 Sitiari ya Kikaida ........ 23
2.1.17 Sitiari hisimseto ........ 23
2.1.18 Sitiari mseto ........ 24
2.1.19 Hitimisho ........ 24
**SURA YA TATU: MATUMIZI YA SITIARI KATIKA UTENZI WA RASI'LGHULI ........ 26**
3.0 Utangulizi ........ 26
3.1.0 Sitiari Kuu ........ 26
3.1.1 Sitiari sahili ........ 43
3.1.2 Sitiari chakavu ........ 50
3.1.3 Sitiari Hisimseto ........ 52

3.1.4 Sitiari ya usuli ........ 54
3.1.5 Hitimisho ........ 61
**SURA YA NNE: MATUMIZI YA TAKRIRI KATIKA UTENZI WA RASI'LGHULI ........ 63**
4.0 Utangulizi ........ 63
4.1 Ufafanuzi wa takriri katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani ........ 63
4.1.1 Takriri Irabu/Vokali ........ 64
4.1.2 Takriri Konsonanti ........ 73
4.1.3 Takriri Neno/Maneno ........ 77
4.1.4 Takriri Silabi ........ 83
4.1.5 Hitimisho ........ 89
**SURA YA TANO: HITIMISHO ........ 91**
5.0 Utangulizi ........ 91
5.1 Malengo ya utafiti wetu ........ 91
5.2 Utathmini wa Nadharia Tete ........ 94
5.3 Mapendekezo ya utafiti ........ 95
MAREJELEO ........ 97

# SURA YA KWANZA

## Utangulizi

Utafiti huu unahusu matumizi ya sitiari na Takriri  katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Utenzi huu ni mmoja wa tenzi za kale silizowahi kuchapishwa. Utenzi huu una beti 4,584 hivyo kuwa ndio mrefu zaidi kuliko zote zilizochapishwa katika lugha yoyote ile ya kiafrika na unasemekana kuwa ni wa pili kwa urefu miongoni mwa tenzi za Kiswahili zinazojulikana. Knappert (1967) anaelezea dhana ya waislamu wa Afrika mashariki kulingana na maelezo aliyopata katika tenzi za kale, ukiwemo *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Utenzi huu uliandikwa katika miaka ya (1850) (kwa mujibu wa Dibaji ya mhariri uk vii) na mpaka leo, kwa ubora wa sanaa yake na kina cha maudhui yake, bado unashikilia nafasi ya pekee katika bahari ya ushairi wa Kiswahili. Mtunzi wa utenzi huu ni Mwalimu Mgeni bin Faqihi kama anavyotueleza katika beti za (25-30). Asili ya utenzi huu ni kisa kimoja cha kiarabu kiitwacho Futuhu 'lyamani (maana yake kushindwa au kutishwa kwa Yemen). Kisa hicho cha kiarabu husimulia jinsi nchi ya Yemen ilivyoshindwa na kutekwa na majeshi ya Waislamu yakiongozwa na Seyyidna Ali bin Abi Talib, Seyyidna Umar bin Khatab na Mtume Muhamadi mwenyewe, kunako karne ya sita. Rasi'lGhuli ambaye jina lake ni Mukhariki bin Shahabu, ndiye mtawala wa 'makafiri' wa Yemen aliyeshindwa na majeshi ya Waislamu. Rasi'lGhuli ni jina la kebehi lenye maana ya 'Kichwa cha Nyoka'.

Utenzi huu husimulia matukio yalioambatana na kuanzishwa kwa uislamu huko Saudi Arabia na Yemeni kunako karne ya saba. Mgongano mkuu ulitokea kati ya mfumo wa fikra, itikadi, mwenendo na mahusiano ya jamii ya Kiislamu, yaliyokuwa yakiasisiwa na Mtume Muhamadi mwenyewe na sahaba zake, na utaratibu wa Rasi'lGhuli na wenzake.

Mgogoro huu na jinsi ulivyoendelezwa katika medani ya vita, katika itikadi na katika mila na ada za watu unahusishwa kwa ubingwa mkubwa katika mchangamano huu wa sanaa na historia ya mtunzi wetu mahiri, Mgeni bin Faqihi.

Pamoja na kwamba *Utenzi wa Rasi'lGhuli* ni miongoni mwa tenzi ndefu na za jadi kabisa katika Kiswahili, hakuna marejeleo muhimu na ya kitaalamu kuuhusu. Katika utafiti wetu, tumechunguza matumizi ya sitiari na takriri katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani.

## 1.1 Usuli

Kabla ya kuja kwa wageni katika pwani ya Afrika mashariki, mashairi na tenzi nyingi zilikuwa zinatungwa na kusimuliwa au hata kuimbwa kwenye sherehe mbalimbali kama vile, arusi, matanga, jando, unyago na tumbuizo za aina tofauti katika jamii nyingi za kiafrika. Mnyapala (1965) anasema kuwa waswahili walikuwa wakifungiana nyama kwa kubuni tenzi na mashairi ili kuwasilisha mawazo yao.

Kulingana na Mlokozi (1999) tenzi ni tungo ndefu za ubunifu ambazo maudhui yake yanajikita katika masuala ya kidini, mbeko, mila, utamaduni na historia. Ushairi andishi ulianza kuandikwa kwa hati za kiarabu tangu karne ya II. Waarabu walipokuja katika mwambao wa Afrika mashariki, walieneza dini ya kiislamu pamoja na tamaduni na mbeko zao. Mambo haya yaliathiri kwa kiwango kikubwa maisha ya waafrika. Kwa mfano uchumi, utamaduni, elimu, siasa, utawala, tabia, mavazi na hata dini.

Baadhi ya waafrika waliweza kuteuliwa kuwa viongozi wa dini, watawala na pia kusoma na kuanza kuandika kwa kutumia hati za kiarabu. Baada ya kuibua usanii wa kuandika, fasihi simulizi ya Kiswahili ilianza kufasiriwa kwa hati za kiarabu. Wageni wengine

waliofuatia baada ya utawala wa Waarabu wa Omani mwishoni mwa karne ya 18, pia walitumia na kuhifadhi fasihi hiyo kwa hati za kireno na hasa katika upwa wa Afrika mashariki.

Allen (1938) anadai kuwa baada ya majilio ya ukoloni katika upwa wa Afrika mashariki na fasihi simulizi kuandikwa kwa lugha za kigeni, tenzi zilianza kufasiriwa na kuandikwa kwa hati za kirumi. Kwa mfano, *Utenzi wa Rasi'lGhuli* uliotungwa na kutafsiriwa na Mwalimu Mgeni bin Faqihi ni miongoni mwa tenzi za zamani zilizotafsiriwa kwa lahaja za Kiswahili kwa sababu ya umaarufu wake.

Dini ya kiislamu iliathiri pakubwa uandishi wa fasihi ya Waswahili. Hii ndio sababu watafiti wengi wa fasihi hii walidai kuwa kama utenzi haungetangulizwa na fomula maalum kama vile sifa za Mungu, Mtume Muhammadi na aila yake, masahaba, masufii na wafuasi wa dini ya kiislamu, basi huenda kuna baadhi ya beti ambazo zimeondolewa.

Steere (1970:39) anasema kuwa tendi nyingi ziliangazia maudhui ya dini ya kiislamu, kwani wengi wa watunzi walikuwa wamesilimu na kuwa wafuasi shupavu wa dini hiyo na hivyo kuathiri maudhui ya kidini. Naye Knappert (1967:49) anadai fomula hii ya utunzi ilizingatiwa na takribani wote wa tenzi za zamani kama inavyoadhihirika katika utangulizi wa tenzi nyingi za kale kama vile *Siri li Asirali*, *Al Inkishafi*, *Fatuma, Tambuka, Siiraji, Rasi'lGhuli* na zingine.

Kwa mfano, katika utangulizi wa *Utenzi wa Rasi'lGhuli*, Mtunzi anaanza kwa fomula hiyo ambayo imezoeleka. Takriban katika Utenzi wa Rasi'lGhuli sifa za Mungu na umuhimu wa imani ya kiislamu zinapatikana katika beti nyingi.

Licha ya hayo waswahili nao walikuwa na mtindo na desturi ya kuwaachia wanao uridhi kwa njia ya wosia. Kulingana na wao kila mlezi alikuwa na wajibu wa kuwausia wanawe kabla ya kuondoka ulimwenguni. Mfano mzuri ni kama vile Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Siiraji, Kiokozi cha Banati, Utenzi wa Adili na Nduguze na zingine. Tungo za kiwosia za kuigwa na wanajamii ili kuyapa maisha yao thamani sio tu kwa kizazi cha wakati huo bali hata kwa vizazi vilivyofuatia baadaye.

Hata hivyo visa vingi pia vilisimuliwa ili kuonyesha ushindi wa Waislamu dhidi ya makafiri. Visa hivi vilikuwa vya vita kama vile katika *Utenzi wa Siri Li Asirali, Tambuka, Fatuma, Rasi'lGhuli* miongoni mwa zingine. Vita hivi vilikuwa vinapiganwa ili kueneza uislamu kwa sababu wale walikubali kusilimu walisamehewa na kuchukuliwa kama ndugu. Mifano mizuri inapatikana katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* kama tulivyo dhihirisha.

Kisa cha Rasi'lGhuli kilikuwa kinapendwa na watu wengi sana. Asili ya utenzi huu ni kisa kimoja cha kiarabu kiitwacho Futuhu 'Lyamani (maana yake kushindwa kwa Yemeni) utenzi huu husimulia matukio yalioambatana na kuanzishwa kwa uislamu huko Saudi Arabia. Hii ndio sababu kukawa na haja ya kutafsiri kwa Kiswahili ili watu wengi wapate kuelewa, Rasi'lGhuli maana yake ni "Kichwa cha Nyoka."

## 1.2 Tatizo la utafiti

Katika utafiti huu tumechunguza matumizi ya sitiari na takriri katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani.

Lugha ya kitamathali huwa na umuhimu mkubwa sana katika utunzi wa kazi za kifasihi.

Wamitila (2003) anaeleza matumizi matatu makuu ya lugha ya kitamathali. Lugha ya kitamathali huwa na jukumu la urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa na lugha hiyo. Pili, lugha ya kitamathali huwa na jukumu la ufafanuaji wa kinachohusishwa na tamathali maalumu. Aidha, lugha ya kitamathali huwa na jukumu la udhabitishaji, yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na udhabiti fulani. Na kwa njia hii mkokotezo mkubwa.

Matumizi mazuri ya tamathali za usemi huipa kazi ya kifasihi mvuto na uzuri wake. Kwa upande mwingine, matumizi mabaya na ulazimishaji wa tamathali za usemi katika utungo fulani huifanya kazi ya kifasihi kuwa duni katika usanii wake na kuupoteza umahiri wake.

Kazi ya mtunzi huhakikiwa ili kupima ufanisi au kutofana kwake katika utunzi wake. Matumizi ya tamathali za usemi huwa ni kigezo muhimu cha kupima ufanisi huo au kutofana kwake. Ingawa kuna wengi walioshughulikia tenzi za kale katika vipengele vya wahusika, maudhui na hata fani kwa ujumla kwa kutumia Nadharia mbalimbali kama Kimtindo,Natorojia na hata Kimuundo wakiwemo; Lugwiri, Arege, Mutiso, Knappert, Abdulaziz na wengineo. Hakuna aliyeshughulikia vipengele vya Sitiari na Takriri kwa kina katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* kama tulivyoshughulikia. Hivyo tumeonelea ni muhimu kuziba pengo hili.

## 1.3 Malengo ya utafiti

Malengo yetu katika tasnifu hii ni:

i. Kutumia uhakiki wa kimuundo kuhakiki sitiari na takriri katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli.*

ii. Kubainisha jinsi tamathali hizi mbili zinavyofanikisha kazi ya mtunzi kifani.

iii. Kueleza na kufafanua dhana za sitiari na takriri pamoja na aina za kila mojawapo na kisha kuzichambua.

### 1.4 Sababu za kuchagua mada hii

Tumechagua mada hii kwa sababu kadha, kwanza hatukupata kazi yoyote ya kihakiki kuhusu mada hii katika nadharia ya umuundo. Arege aligusia kidogo tu kwa kutumia nadharia ya Natorojia. Wengine ni kama wa Mutiso, Knappert, Allen, Abrahams na Reinehart na Winston. Pili *Utenzi wa Rasi'lGhuli* haujashughulikiwa na wasomi wengi labda kwa sababu lugha iliyotumiwa ni chakavu na hivyo haieleweki na wengi. Aidha kuna mseto wa msamiati wa Kiarabu, kingozi na lahaja nyinginezo. Mutiso (1996:5) .Hivyo kuna haja kubwa ya uhakiki wa kitaalamu wa utenzi huu kwa upande wa vipengele vya matumizi ya lugha ili kurahisisha uelewekaji wake.

Tatu tumechagua utenzi huu kwa sababu ni miongoni mwa tenzi za kale zilizowekea msingi ushairi unaotumika hata leo. Baadhi ya tungo hizo zikiwemo *Utenzi wa Hamziyah, Siri li Asirali, liyongo, Mikidadi na Mayasa, Fatuma naTambuka.* Hivyo kuna pengo kubwa la kiusomi katika kipera cha tenzi ambalo linapaswa kuzibwa. Hatua la kuliziba pengo hili itachangia pakubwa katika jitihada za kukuza na kuiendeleza fasihi andishi changa ya Kiswahili. Vilevile tunadhamiria kuwapa changamoto wasomi na wahakiki chipukizi wa Kiswahili kutazama upya matumizi ya tamathali za usemi na nafasi yake katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni utunzi wake wa hali ya juu wa kisanaa unaopatikana katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli.* Mtunzi amewasilisha sitiari na takriri kwa njia ya kiueledi. Na hivyo kutufanya kuwa na hamu na ghamu ya kutaka kuangazia matumizi yake kama njia moja ya kumbukizi za usanaa wake.

Kwa ujumla sababu zetu za kuchagua somo hili zimechangiwa na shinikizo za kiusomi. Ni matumaini yetu kuwa utafiti huu utasaidia pakubwa katika hazina ya uhakiki wa tenzi za Kiswahili za jadi, ambazo kulingana na Mutiso (1996:5) zinaogopwa na wanafunzi wengi hata wale ambao Kiswahili ni lugha yao ya kwanza. Kwa hivyo tunawapa changamoto wasomi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kuhakiki vipengele vingine vya fasihi mbali na takriri na sitiari katika kazi zingine za kale.

## 1.5 Upeo na mipaka

Uhakiki huu umetathimini matumizi ya tamathali za usemi ambazo ni sitiari na takriri katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani. Tumejadili dhana ya sitiari na aina zake na dhana ya takriri na aina zake pamoja na uamilifu wa aina hizi za kitamathali katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani katika utenzi huu.

Tumejikita katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* kama unavyohitaji mwelekeo wa kihakiki wa umuundo. Tumejadili namna vipengele hivi vya kifani vilivyotumiwa, uamili wake wa kiumbuji na mchango wake katika muundo wa kazi nzima.

Tumedurusu kazi mbalimbali za wasomi wengine ili kuelewa maoni yao kuhusu vipengele hivi vya fani. Baadhi ya Tenzi hizi ni *Al Inkishafi*, *Liyongo*, *Fatuma*, *Tambuka Siri li Asirali*, *Mikidadi na* Mayasi na zingine. Hata hivyo tumechukua mwelekeo wetu wa kuchambua na kuwasilisha kazi yetu.

## 1.6 Nadharia tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete mbili kuu:

i. *Utenzi wa Rasi'lGhuli* una matumizi mengi ya sitiari na takriri yanayodhihirisha umbuji wa hali ya juu.

ii. Mbinu hizi mbili zimesheheni katika utenzi wote kutoka mwanzo hadi mwisho, hivyo kudhihirsha umuhimu wake katika kuendeleza hadithi pamoja na kufanikisha matumizi ya fani.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii

Uchunguzi wetu kuhusu yalioandikwa kuhusu somo hili umejikita katika ushairi wa Kiswahili na hasa katika mashairi ya jadi yalioandikwa kabla ya karne ya ishirini. Hii ni kwa sababu utenzi wetu uliandikwa wakati wa kipindi hicho. Mengi yameshughulikiwa kuhusu dhana ya maudhui, wahusika na fani katka tenzi mbalimbali za kifasihi za Kiswahili. Wataalamu wa kigeni waliofanya utafiti katika tenzi za kale ni pamoja na Knappert (1967, 1971, 1979), Lambert (1965) Culler (1975) na Harries (1962) . Wahakiki hawa wa kigeni hawakuona tofauti kati ya utamaduni wa Kiswahili, Waislamu na itikadi ya dini ya kiislamu iliyoenea eneo la Afrika Mashariki.

Trimingham (1964) anaunga mkono wazo hili kwa kusema kuwa "mtu aliyesilimu alibaki kuwa mwafrika hata kama ilimbidi afuate mbeko za uislamu kama vile "faradhi" na "Sunna". Tabia kama hizi za kidini hazikuasi mila na desturi ya kiafrika, kwani zilijidhihirisha katika kazi yao ya usanii wa kimaandishi, hasa nyimbo za jandoni, unyagoni, mashairi na tenzi. Hata hivyo, wengi wa wasomi wa fasihi ya Kiswahili wanaonekana kupuuza mchango wa watafiti hawa katika fasihi ya Kiswahili.

Kwa mfano, Kezilahabi (1997:59) anadai "…Wale wataalamu wa kizungu ambao wamejitahidi sana na kukiendeleza na kukikuza Kiswahili walikuwa na ujuzi mdogo sana wa fasihi. Wao walikuwa wataalamu wa lugha na hawakuweza kufanya lolote zaidi ya kukusanya maandishi kadha ya Kiswahili na kuyatafsiri katika lugha zao kwa manufaa yao wenyewe kwa upande wa lugha, walifanya mambo mengi mazuri."

Allen (1971) alikusanya mashairi sita ya kale ambayo alitafsiri kwa kiingereza na kutengeneza makala mafupi. Haya ni pamoja na *Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Ngamia na Paa. Utenzi wa Masahibu, Utenzi wa Mikidadi na Mayasa. Utenzi wa Ayubu na Utendi wa Kiyama*..

Hata ingawa mashairi haya na makala hayana uhusiano wa moja kwa moja na kazi yetu, kuna sehemu ambazo zinahusu chanzo na itikadi za mashairi ya kale ambayo yatakuwa muhimu katika kazi yetu. Allen anatambua kuwa kuna miswada michache ambayo inaweza kupatikana ya miaka kabla ya karne ya kumi na nane. Anasema kuwa miswada inayopatikana ni mfano wa miswada ya kale kwani baadhi ya maneno asili yametolewa au kuachwa na mengine kuongezewa.

Kwa upande wetu, watafiti hawa walifanya jambo la maana sana kwani waliwekea msingi imara utafiti katika tenzi za Kiswahili. Pamoja na utafiti wa wageni, kuna uhakiki uliofanywa majuzi kuhusu tenzi za kale na wasomi kama vile Wa Mutiso (1996),"*Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry; Kasida ya Burudai*". Wa Mutiso (2003): *Analysis of Swahili Poetry; Five Swahili Epic by four Swahili Women*, (haujachapishwa), Abdulaziz (1979) *Muyaka 19th century Swahili Popular Poetry*. Mulokozi, (1999) *Tenzi Tatu za kale*, Dar-es-Salaam: Tuki, Tom Olali (2004) *The*

*Veneration of the Prophet: The Role of Kasida Hamziyya. During the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya. Tasnifu ya PHD (haujachapishwa)* Mungai P.K. (2005) "*Uhakiki linganishi wa kifani wa tenzi Mikidadi na Muyaka na swifa ya Nguvumali*" (haujachapishwa) Okombo Lugwiri (2011) "*Sitiari*, *Taashira na tashbihi katika uandishi wa dhana katika Utenzi wa Tambuka*"(mswada ambao haujachapishwa). Arege (2012) *Narration in Swahili narrative poetry: an analysis of Utenzi wa Rasi'lGhuli* (mswada ambao haujachapishwa). Hata hivyo hatukupata kazi yoyote ya kihakiki iliyoshughulikia *Utenzi wa Rasi'lGhuli* kwa kina kwa upande wa sitiari na takriri. Labda ni kwa sababu ya urefu wa utenzi wenyewe na lugha ambayo haieleweki kwa urahisi. Maelezo mengi ya kimsingi yameelezwa na Mutiso (1996) na yametufaa sana katika kazi yetu. Pia ndiye aliyetupatia *Utenzi wa Rasi'lGhuli* ambao tumetumia katika uchambuzi wetu.

Kuna pengo kubwa la kiusomi katika kipera cha tenzi ambalo linapaswa kuzibwa. Hatua la kuliziba pengo hili litachangia pakubwa katika jitihada za kukuza na kuiendeleza fasihi andishi changa ya Kiswahili.

### 1.8 Mbinu za utafiti

Utafiti huu umekuwa wa maktaba. Tumesoma mashairi na tenzi mbalimbali za kale. Tumerejelea tasnifu, vitabu, majarida na machapisho mengine ambayo yana makala yaliyotusaidia katika utafiti wetu. Pia tumesoma kuhusu nadharia ya umuundo na kubainisha sifa zake kutoka maktabani. Tulitumia yaliyomo katika mtandao kuhusu nadharia yetu ya umuundo. Hatimaye tulianza uchambuzi wa *Utenzi wa Rasi'lGhuli* ambao ni wa kale na haujatafitiwa kwa kina kwa upande wa takriri na sitiari.Hata hivyo

tulipata ushauri mbalimbali kutoka kwa wahadhiri tofauti ambao umekuwa wa maana na usaidizi mkubwa kwetu.

## 1.9 Msingi wa nadharia ya utafiti

Nadharia ambayo tumetumia katika utafiti huu ni ya umuundo. Nadharia hii imetusaidia sana katika kuchanganua tamathali za usemi ambazo ni sitiari na takriri katika kufanikisha kazi ya mtunzi wa *Utenzi wa Rasi'lGhuli* kifani.

Nadharia ya umuundo iliibuka nchini Czechoslovakia mwishoni mwa miaka ya ishirini. Kwa mujibu wa Earlich (1969) nadharia ya umuundo inahusishwa na wana-isimu wa shule ya Prague kati ya miaka ya (1928-1946) ambao walihusika na urasimu wa Kirusi kabla ya kuanguka kwake. Pia anaendelea kueleza kuwa kuzuka kwa shule ya Isimu ya Prague kulihusishwa sana na urasimu na hasa kikundi kimoja cha wana-isimu wa Moscow.

Baadhi ya waasisi wa nadharia ya umuundo ni Roman Jakobson, N.S. Trubetzekoy, Borris Tomaserky, Jan Kukarovsky na Wellek. Culler (1975:4-5) anaelezea kuwa waasisi wa umuundo walitumia mawazo ya mwana-isimu Ferdinand de Saussure ambaye alibuni dhana mbalimbali za kiisimu na akawafundisha wanafunzi wake kupitia kwa mihadhara mbalimbali. Mawazo ya De Saussure yalichapishwa na wanafunzi wake wakiongozwa na Charles Barry (1916)'A Course in General Linguistic'.Cambridge; Cambridge University Press.

Dhana zilizobuniwa na Saussure ni pamoja na 'Langage' (Lugha ijulikanayo na kutumiwa na jamii) 'Langue' (sheria na kanuni za lugha) na "Parole" (matumizi ya lugha katika mazungumzo na maandishi) wanaumuundo walitumia dhana hizi kusisitiza kuwa,

ili kuelewa mfumo wa kazi ya kifasihi, mhakiki anafaa kuchunguza matumizi ya lugha katika maandishi au mazungumzo, vipengele vyake na mahusiano yake. Wanaumuundo walieleza kuwa fasihi ni mfumo unaojisimamia kama 'Langue' na una kaida zake. Hivyo, kazi ya kifasihi inafaa kuangaliwa kwa mujibu wa kanuni bia za utanzu zinazoitawala. Kwa mfano, katika kuhakiki *Utenzi wa Rasi'lGhuli* sharti tuchanganue tamathali za lugha kama vile sitiari na takriri zilizotumiwa na vilevile sheria au kaida zinazotawala utunzi wa utenzi na kuona ikiwa mtunzi alitekeleza hizo sheria.

Waasisi wa umuundo walichunguza mbinu za kifani kama vile jazanda, taswira, tashihisi, sadfa, sitiari, takriri na ukiushi. Walieleza kuwa matumizi ya hali ya juu ya mbinu hizi huitofautisha lugha ya kifasihi na lugha ya kawaida na taaluma nyingine.

Wanaumuundo walieleza kuwa kufaulu kwa kazi ya kifasihi hutokana na mbinu za kifani ambazo mtunzi anazitumia. Waasisi wa umuundo walijali zaidi muundo wa kazi ya kifasihi kuliko mandhari ya kijamii ya kazi hiyo. Pia walipuuza kuhusisha fasihi na mtunzi wake.

Waanzililshi wa umuundo walihakiki mashairi na tungo zingine za kifasihi. Walichunguza upatanifu wa sauti, vina, mizani, kiimbo, wizani na arudhi kwa jumla. Katika tungo za kimasimulizi, walisisitiza umbo la msuko, hadithi na umbuji wa wahusika.Hii ndio sababu tulichagua kuchunguza matumizi ya sitiari na takriri na jinsi zilivyochangia katika kufanikisha vipengele hivi vyote kwa jumla katika *Utenzi wa Rasi 'lGhuli .Pia walisisitiza hali ya ubunifu katika matumizi ya lugha walipendekeza mbinu za ukiushi katika matumizi ya lugha..Walipendekeza mbinu za ukiushi katika matumizi ya lugha kama vile tamathali za usemi.*

Nadharia ya umuundo imetusaidia sana katika Utenzi huu katika uchanganuzi wetu, kwa kuwa inatilia mkazo muungano na mwingiliano wa vipengele mbalimbali vya kifani katika ujenzi wa kazi ya kifasihi. Hivyo imeafiki malengo yetu katika utafiti huu.

### 1.10 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili juu ya tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na sababu za kuchagua somo. Pia tumeshughulikia upeo na mipaka ya utafiti, yalioandikwa kuhusu somo na msingi wa nadharia ambayo ni umuundo na mwishowe tukajadili njia tulizozitumia katika utafiti wetu ambapo tumejikita sana maktabani, kuwauliza wataalamu mbalimbali wakiwemo wahadhiri wetu wa Chuo Kikuu cha Nairobi na pia kurejelea mtandao.

Mchango wa wataalamu wa fasihi pia umetufaa sana. Tumewashirikisha wahadhiri wetu pamoja na wasomi wengine ili kuboresha kazi yetu.

# SURA YA PILI

# MAELEZO YA KIMSINGI YA DHANA YA TAKRIRI NA SITIARI

## 2.1.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia mambo ya kimsingi juu ya utafiti wetu. Mambo hayo yamekuwa msingi muhimu uliotuongoza katika kuelezea zaidi utafiti huu. Katika sura hii ya pili, tumejikita katika misingi ya kinadharia ya takriri na sitiari, pamoja na aina ya kila mojawapo ya tamathali hizo za usemi. Tumetolea mifano mahsusi ya kijumla ili kusaidia kueleweka kwa kazi yetu. Tumerejelea dhima ya kijumla ya tamathali zote mbili katika matini za kifasihi na pia maelezo katika mtandao, waandishi na wahakiki mbalimbali wa fasihi.

Tamathali hizi za usemi zina uhusiano wa karibu kwa kuwa zinachangia pakubwa katika kuipamba lugha na kuifanya ya kuvutia na yenye mnato wa hali ya juu, sio tu katika kazi ya msanii bali pia kwa hadhira. Tamathali zenyewe zinapatikana katika kategoria ya kisarufi ya semantiki.

## 2.1.1 Dhana ya fani

Fani ni vipengele vya kisanii vitumiwavyo kuyawasilisha maudhui. Bali na kuyawasilisha maudhui, fani pia huwa na uamilifu wa kuupa utungo wa kifasihi umbo mahsusi. Umbo lenyewe linaweza kuwa la ndani au nje. Katika tungo za kishairi, umbo la ndani hujengwa kwa vipengele vya fani kama vile matumizi ya lugha, wahusika, mandhari, msuko, usimulizi, toni na kadhalika. Kwa upande mwingine umbo la nje hujengwa kwa vipengele vya fani kama vile beti, mishororo, mizani na vina.

Wataalamu na wahakiki wa fasihi kama vile Mutiso (2005), Mbatiah (2001) na Wamitila (2003). Wanakubaliana kuwa fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Nao wataalamu wa nadharia ya umuundo wanasisitiza na kutilia mkazo uhakiki wa kifani katika kufasiria matini na kupimia kufana au kufeli kwa mtunzi katika kazi yake ya usanii. Utafiti wetu umechunguza jinsi matumizi ya sitiari na takriri yalivyochangia katika kufanikisha vipengele hivi na vingine.

### 2.1.2 Tamathali za usemi

Tamathali za usemi huchukua nafasi kubwa na muhimu katika uchanganuzi wa lugha ya kifasihi. Tamathali za usemi huwa ni mojawapo ya mbinu za matumizi ya lugha ya mkato na ya kisanii na humwezesha mtunzi kusema mengi kwa maneno machache yenye mvuto, mguso na mnato.

Dhana ya tamathali za usemi si ngeni katika taaluma ya fasihi. Dhana hii imewahi kuelezewa na kufafanuliwa na waandishi na wahakiki mbalimbali wa fasihi ya kimagharibi na vile vile wa fasihi ya Kiswahili. Waandishi wa kimagharibi waliozungumzia kuhusu dhana hii ni pamoja na Holman (1936) Fowler (1973) Abrahams (1941) Frye na Perkins (1985) Holman na Harmon (1986) na Wales (2001) miongoni mwa wengine.

Uchanganuzi wa kina kuhusu dhana ya tamathali za usemi katika Kiswahili unapatikana katika Kuhenga (1977) na Wamitila (2008).

Kwa kuzingatia maelezo ya wataalamu hawa wa fasihi, tunaweza kuelezea tamathali za usemi kama wanavyozielezea Holman na Harman (1986:2002) kuwa ni matumizi

mbalimbali ya lugha ambayo hukiuka mtindo uliozoeleka ili kuleta athari au maana fulani.

Matumizi ya lugha kwa namna hii huenda kinyume na kile ambacho wazungumzaji wa lugha fulani wanakielewa kuwa kawaida, wastani na yenye mpangilio wenye ruwaza ya maneno.

Tamathali za usemi hazipatikani tu katika fasihi, bali hutumika kwa wingi katika mazungumzo ya kila siku. Wengi wa wazungumzaji wa kila siku hutumia mojawapo au ziadi ya mbinu za kitamathali bila kujua au kutarajia. Hapa pana maana kuwa baadhi ya maneno katika lugha nyingi yana asili yake katika tamathali za usemi.

Tamathali ambazo tumeshughulikia ni mbili. Nazo ni takriri na sitiari. Hii ni kwa sababu zimetumika kwa wingi katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Kwa hivyo tumechunguza umuhimu wake, sababu za kutumika kwa wingi na jinsi zilivyotumika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani.

### 2.1.3 Takriri

Neno takriri limetoka kwa neno la Kiswahili 'kukariri'. Katika kamusi ya kiswahili kukariri maana yake ni kusema tena na tena maneno yale yale kimoyomoyo au kwa sauti. Katika kauli hii neno takriri limetumika kwa maana ya kuthibitisha kwa kurudiarudia.

Wamitila (2008) Takriri ni mbinu inayorejelea urudiaji wa sauti, neno au sentensi fulani, pia hujulikana kama uradidi. Kwa maoni yetu takriri ni mbinu ambayo hutumika na mtunzi kurejelea urudiaji wa sauti fulani, herufi, maneno au mstari fulani katika kazi za kifasihi. Nia ya mtunzi anapotumia mbinu hiyo huwa ni kuleta msisitizo katika ushairi wa kimapokeo wa kiswahili. Takriri inayojitokeza sana ni ile ya vina, ambapo sauti

fulani inarudiwa katika mishororo ya shairi.  Takriri pia inaweza kuwa ya sauti au ikawa ya maneno.

Kwa mujibu wa Kuhenga  (1977) Takriri ni mtindo wa uneni wa fasaha ambao msemaji kwa makusudi au nia mahsusi hurudia neno au maneno yale yale ili kutia mkazo au msisitizo zaidi juu ya jambo asemalo, mtindo huu wa msemo wa msistitizo huwa na nia ya kutia nanga jambo fulani ili liweze kumwingia msikilizaji moyoni apate kulithibiti vizuri.

Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa takriri ni mbinu ya kisauti au maneno ya kurudia irabu, konsonanti, silabi au neno katika utungo fulani. kwa nia ya kusisitiza na kuweka udhibiti moyoni ili lisisahaulike.Hata hivyo kwa maoni yetu pia mtunzi anaweza kutumia takriri ili kupunguza idadi ya maneno kwa nia ya kurahisisha uelewekaji wa kazi yake na hasa ikiwa Utenzi ni mrefu kama ilivyo katika *Utenzi wa Rasi lGhuli*.

### 2.1.4 Aina za Takriri

Zifuatazo ni baadhi ya aina za takriri ambazo zimetusaidia katika uchanganuzi wa *Utenzi wa Rasi'lGhuli.*

### 2.1.5 Takriri Irabu/Vokali

Ni hali ya kurudia irabu ile ile katika sehemu sawia za neno katika sentensi.  Athari ya takriri irabu ni kuleta wizani au ridhimu katika utungo wa kifasihi hasa katika ushairi. Mfano mzuri unapatikana katika tenzi za kale *kama Utenzi wa Fatuma, Siri li Asirali, Utenzi wa mwanakupona* miongoni mwa nyingine.

Wamitila (2003) anasema kuna uwezekano ikawa kurudia kunakojitokeza ni matokeo ya sifa za lugha inayohusika tu, bali si tendo la kimakusudi la mwandishi fulani.

### 2.1.6 Takriri Konsonanti

Wamitila (2003) anaeleza kuwa istilahi hii hutumiwa kuelezea urudiaji wa sauti ya konsonanti. Kimsingi kurudia huku hutokea mwanzoni lakini inawezekana kupatikana pengineko. Muhimu ni kuwa kurudia huku kunajitokeza wazi. Katika ushairi wa kiswahili, takriri irabu na takriri konsonanti hazijitokezi sana kama katika kiingereza kwani kiswahili hupendelea muundo wa konsonanti kufuatwa na irabu. Kwa mfano, katika Utenzi wa Rasi ‘lGhuli kuna maneno kama : himahima, mivumbimivumbi, tamutamu na tungutungu. Mifano zaidi hupatikana katika tungo za kale za ushairi.

### 2.1.7 Takriri – Neno / Maneno

Aina hii ya takriri hutumiwa kuelezea urudiaji wa maneno au neno fulani katika matini au kazi fulani.

Hii ni njia mojawapo ya kusisitiza jambo au hata kuchezea maneno ya utungo wenye takriri. Maneno yanaweza kuwa pia na wasifu wa tauria (mchezo wa maneno yanayofanana) kwa mfano katika *Utenzi wa Rasi’lGhuli* maneno kama ‘baada’ ubeti wa 54 na 55 na wakati mwingine ‘baadaye’ yametumika kwa wingi na pia ubeti wa (3555) neno unasi, ajinasi ajinasi limerudiwa kwa wingi. Maneno mengine ni kama; achenenda, habari, kufari na khatari.

### 2.1.8 Takriri Silabi

Takriri silabi ndiyo aina ya urudiaji ambayo inapatikana kwa wingi katika tungo za kishairi. Silabi zinazorudiwa mara nyingi huwa muungano wa konsonanti na vokali. Takriri silabi imetumiwa katika vina vya mishororo ya kila ubeti katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli.*Vina vya mishororo ya kwanza mitatu vinarudiwa katika utenzi wote na vina fanana.

Vile vile kina cha mshororo wa mwisho wa kila ubeti kinarudiwa katika mishororo yote ya mwisho katika utenzi mzima. Mbali na takriri zinazohusu vina kuna takriri ambazo pia zinahusu silabi za kuanzia mishororo ya beti. Baadhi ya beti katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* zina takriri ya aina hii .Mfano : ubt.1075, 549,560,731 na 982.

### 2.1.9 Ufafanuzi wa sitari kama tamathali ya usemi

Sitiari ni mojawapo wa semi linganishi tabia. Sitiari ni neno lililozaliwa kutoka kwa neno 'sitiri'. Kusitiri maana yake ni kuficha au kufunika, kwa hivyo sitiari maana yake ni namna ya kifuniko au kitu chenye kuficha. Wasomi wengi wameandika mengi juu ya tamathali hii ya usemi. Kulingana na Myers na Simms (1989:178), neno sitiari lina asili yake katika lugha ya Kigiriki na lina maana ya 'kuhamisha' au 'kuvusha' hadi upande mwingine. Kutokana na maelezo haya ya Myers na Simms, tunaweza kueleza sitiari kama tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kulinganisha vitu viwili tofauti au vyenye tabia tofauti bila kutumia viungo vinavyotumiwa katika tashbihi. Katika sitiari ulinganisho huwa wa moja kwa moja. Kitu kimoja hutajwa kuwa kingine. Hii ina maana kuwa, maana ya msingi ya kitu ambacho hutajwa hukiukwa. Maana inayorejelewa huwa ni maana ya kipragmatiki.

Muundo wa kijumla wa sitiari huwa na sehemu tatu: sehemu ya kilinganishi, kilinganishwa na msingi wa ulinganishi Wamitila (2008:420). Kilinganishi huwa ni kitu kinachotumiwa kufananisha na kingine. Kilinganishwa ni kile kinacholinganishwa ilhali ulinganishi ni ile sifa, hulka au hali fulani ya kitu kinacholinganishwa: mfano: Ndumbu ni Yesu wangu (kilinganishi hapa ni 'Yesu' na kilinganishwa ni 'Ndumbu' na msingi ni sifa ya ukombozi, upole, utu wema ambao Yesu huhusishwa nao').

Ujana ni moshi, ukenda haurudi tena, katika mfano huu kilinganishi ni 'moshi' na kilinganishwa ni 'ujana' ilhali msingi ni ile hali ya kutorudi kwa maana ya kuwa hakuna kurudi nyuma katika sehemu uliyotoka.

Fiumara (1995:2) anasema kwamba, katika jadi ya uyunani na urumi, lugha ya kisitiari ilitengewa watawala, matajiri na waajiri. Fiumara anaendelea kueleza kuwa watumwa hawakuruhusiwa kuzungumza kwa lugha ya kisitiari kwani ingekuwa sawa na kupingana au kushindana na waajiri wao. Maelezo haya yanathibitisha kuwa siitiari ilipewa nafasi muhimu katika fasihi ulimwenguni tangu enzi za nadharia ya balagha za zamani katika jadi ya urumi na uyunani.

Davidson (1978) anadai kuwa sitiari nyingi huwa urongo. Maoni yake yanaungwa mkono na Habwe (1999:65) anapoeleza kuwa sitiari ni za urongo kutokana na sababu kuwa zinavunja 'kanuni ya ukweli' katika mawasiliano kama ilivyoelezewa na Grice (1975). Hata hivyo, ingawa tunakubaliana nao kwa kiasi fulani, maoni yetu ni kuwa sitiari ni mbinu ya sanaa inayochangia pakubwa katika kuifanya kazi ya fasihi kuvutia na kuwa na mnato wa hali ya juu, hivyo mara nyingi inapotumiwa kulinganisha mtu au kitu tunachorewa picha ya sifa na umuhimu wake.

### 2.1.10 Aina za Sitiari

Kuna aina nyingi za uainishaji wa sitiari kulingana na wasomi mbalimbali. Tumechagua baadhi ya aina za sitiari ambazo zimetusaidia katika kuchanganua kazi yetu.

### 2.1.11 Sitiari kuu

Ni aina ya sitiari ambayo hutawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Sitiari ya aina hii hurudiwarudiwa au kurejelewa na mtunzi kila mara na hujitokeza kuwa motifu. Jukumu la sitiari kuu ni kuwasilisha dhamira na maudhui ya kazi ya kifasihi. Kwa hali hii, sitiari ya aina hii huwa muhimu katika kuifasiri kazi inayohusika. Sitiari za aina hii ni nyingi katika tenzi za kiswahili. Mfano mzuri ni sitiari ya *simba* katika *Utenzi wa Rasil'lGhuli*. Katika utenzi huu, Shekhe Ali anajisifu kwa kusema **' ndimi simba maarufu '** (120) kumaanisha yeye ni mkali na jasiri kama simba.

Mifano mingine inapatikana katika mashairi huru ya Kithaka wa Mberia, *Bara Jingine* mfano, neno **nyuki** limetumiwa kama sitiari ya waafrika ambao waliungana na kujikomboa lakini baadaye wakapoteza umoja wao na hivyo kuzuia kupatikana kwa maendeleo barani Afrika.

Mfano ulio bora zaidi ni sitiari ya 'Munga' au 'Manga' katika *Utenzi wa Mwana Ninga.* Fumo Liyongo anamlinganisha mpenzi wake na mti wa Munga ambao huwa mrefu na wenye bapa jororo.(Lugwiri 2009).

### 2.1.12 Sitiari Sahili

Aina hii ya sitiari huwa nyepesi na rahisi kueleweka na hadhira. Hii ni kwa sababu ulinganishi wake ni wa moja kwa moja. Mfano tuliotoa wa 'Ndumbu ni Yesu' ni aina ya

sitiari sahili na ambayo ni rahisi kueleweka kutokana na sifa za Yesu kuwa mkombozi, mwenye utu, mpole na mpenda amani. Mifano zaidi ni kama ujana ni moshi, yeye ni 'sungura', mimi ni 'kinyonga' kumaanisha tabia ni kama za mnyama anayetajwa. Aina hii ya sitiari imetumika katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* kwa wingi.

### 2.1.13 Sitiari Chakavu

Murray (1978 :85) anadai kuwa uchunguzi wa sitiari chakavu katka lugha unaweza kutueleza kuhusu maisha ya kijamii na ya kihistoria ya jamii fulani. Naye Abrahams (1957 :64) anaeleza kuwa sitairi chakavu imetumiwa sana katika lugha kwa kiasi cha kuifanya kutoonekana kama sitairi tena. Sitiari za aina hii huwa zimefungamana sana na matumizi ya kawaida ya lugha na hivyo kupoteza ubunifu wake. Aina hii ya sitiari itumiwapo, huwa haina athari zozote za kisanii kwa hadhira katika lugha ya Kiswahili, mifano mizuri ya sitiari za aina hii inapatikana katika misemo na nahau. Mifano ni kama kiuno cha nyingu, shingo la upanga, mdomo wa chupa, meno ya msumeno, mkono wa birika, kichwa cha nyoka na kadhalika.

### 2.1.14 Sitiari ya usuli

Sitiari za aina hii zinapatikana katika lugha nyingi ulimwenguni. Wamitila (2008 :423) anaeleza kuwa sitiari ya usuli ni ''…sitiari ambayo imefungamanishwa na lugha kiasi kwamba watu au wazungumzaji na watumiaji wa lugha hawaiangalii tena kama sitiari au hawafikirii tena kama ni sitiari''. Nyingi ya sitiari za usuli zinapatikana katika utamaduni mahsusi ilhali zingine ni bia, kwa mfano, ''mtihani huu ni 'mboga'' kumaanisha ni rahisi. Akili ni nywele, shilingi ya ua, maisha ni safari, pesa ni maua na kadhalika.

### 2.1.15 Sitiari radidifu

Aina hii ya sitiari si rahisi kueleweka kwani kilinganishi, kilinganishwa au msingi haviwekwi wazi bali ni kutokana na maelezo yake ndipo maana ya sitiari hiyo huweza kufasiriwa na kueleweka. Mfano mzuri unapatikana katika *Utenzi wa mwana Munga* ambapo kulingana na maelezo ya mwandishi mtunzi alishiriki ngono na mwana Munga kwa kulinganisha na shughuli za baharini. Pia katika *riwaya ya Bin-adamu* mbinu hii imetumika kwa wingi.Kwa mfano ; Huntha wa tatu, vizuu na PP.

### 2.1.16 Sitiari ya Kikaida

Kwa kuwa kazi ya fasihi ni zao la jamii, sitiari hii hufungamana na utamaduni wa jamii. Kila jamii au kundi la watu huwa na mambo fulani wanayothamini na hivyo huwa na njia ya kisitiari ya kuyarejelea. Kwa mfano ''mwanamke ni nguo''. Sitiari hii inamaanisha kwamba mwanamke yeyote akipambwa kwa nguo nzuri atakuwa wa kupendeza au mrembo. Mfano mwingine ni kama elimu ni ngao, kumaanisha ukiwa na elimu huna kinga ya maisha kwani unaweza kuajiriwa na kuwa na mali pia unaweza kutumia elimu kujikinga kwa kujieleza.

### 2.1.17 Sitiari hisimseto

Aina hii ya sitiari hutumika kuhamisha hisia za kitu kimoja kwa kitu kingine. Kwa mfano 'Ujumbe Mzito' kumaanisha ujumbe aliobeba ama unaopatikana katika matini fulani una maudhui muhimu. Mifano mingine ni kama 'sauti nyororo' sauti inapewa sifa za wepesi na kuvutia, 'baridi kali', 'upepo mwanana' na kadhalika. Mutiso (1996 :123) anaelezea kuwa kawaida 'giza' linahusishwa na uoga, kushindwa, upweke, msiba, mashetani, mizuka, wanyama wala watu, uchawi, ujinga miongoni mwa mambo mengine

hasi. Kwa upande mwingine moto unahusishwa na hatari na maangamizo. Nayo baridi inahusihwa na upweke na ukosefu wa furaha.

### 2.1.18 Sitiari mseto

Huu ni mchanganyiko wa sitiari zaidi ya moja. Sitiari kadha zinaweza kutumiwa pamoja ili kurejelea hali moja. Sitiari hizi huwa tofauti lakini huwa zinachimuza sifa fulani ya pamoja kuhusu kinacholinganishwa kwa mfano : '*Tabia njema* ni mzizi mkuu wa fadhila. Unapotaka kutafuta mchumba wa kuoa kumbuka *mapenzi ni kikohozi* na pia ni *majani huota popote*. Angalia sana tabia kabla ya kuposa *kwani kuingia ni rahisi kutoka ni ngumu'*.

Katika mfano huu maneno hayo matatu yamelinganishwa ingawa ni tofauti yaani tabia njema, mapenzi kama kikohozi na pia majani. Mathalani mapenzi yamelinganishwa na kikohozi na pia majani. Mke anayechangua anatakiwa kuwa na tabia njema na pia mwenye mapenzi ya wazi ambayo hayafichiki na yanaweza kuanza mahali popote na wakati wowote. Kwa hivyo achunge asihadaiwe na mapenzi na kusahau kuangalia tabia.

### 2.1.19 Hitimisho

Katika sura hii ya pili tumeshughulikia kwa undani maana ya sitiari kwa kurejelea wasomi mbalimbali katika maktaba. Pia tumeelezea aina mbalimbali za sitiari zikewemo sitiari kuu, sitiari sahili, sitiari chakavu, sitiari ya usuli, sitiari radidifu, sitiari ya kikaida, sitiari hisimseto na sitiari mseto. Tumeelezea kila aina na kutolea mifano.

Vilevile tumeelezea takriri kama tamathali ya usemi kwa kurejelea maelezo ya wasomi mbalimbali pamoja na maelezo yetu. Tumeorodhesha na kuelezea aina za takriri na

matumizi yake pamoja na kutolea mifano mwafaka. Aina hizi ni kama takriri – irabu/vokali, takriri konsonanti, kakriri neno/maneno na takriri silabi.

Sababu za kuchanganua tamathali hizi mbili za usemi kwa kina ni kuiwekea msingi kazi ambayo tumeshughulikia. Tamathali hizi zimetumika kwa wingi katika *utenzi wa Rasi'lGhuli* na kwa hivyo msingi huu utakuwa na msaada kwetu.

# SURA YA TATU

# MATUMIZI YA SITIARI KATIKA UTENZI WA RASI’LGHULI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tuliwekea msingi kazi yetu kwa kurejelea kwa kina misingi ya kinadharia ya mbinu zote mbili za matumizi ya lugha yaani takriri na sitiari. Takriri na sitiari ni mojawapo ya viambajengo vikuu katika ushairi wa kale.

Katika *Utenzi wa Rasi’lGhuli* takriri na sitiari zimetumika kwa wingi na kwa hivyo tumezichunguza vile zimetumika na kama zimeweza kufanikisha kazi ya mtunzi kifani. Katika sura hii ya tatu tumejikita katika uhakiki wa matumizi ya sitiari na mchango wake katika kufanikisha kazi ya mtunzi wa *Utenzi wa Rasi’lGhuli* kifani. Katika uhakiki wetu tumegusia uamiri mwingineo wa kisanii wa sitiari uliojitokeza katika utenzi wenyewe. Tumetoa mifano kabambe kutoka katika beti mbalimbali katika utenzi huu, pamoja na kunukuu baadhi ya mifano ili kutilia mkazo maelezo yetu pamoja na kuthibitisha ukweli wa maelezo yetu.

### 3.1.0 Sitiari Kuu

Katika sura ya pili tulielezea sitiari kama mojawapo ya semi linganishi tabia. Sitiari ni neno lililozaliwa kutoka kwa neno “sitiri”, kusitiri ni kuficha au kufunika. Kulingana na Myers na Simms (1989:178) neno sitiari lina asili yake katika lugha ya kigiriki na lina maana ya ‘kuhamisha’ au ‘kuvusha’ hadi upande mwingine. Kutokana na maelezo haya ya Myers na Simms, tunaweza kueleza sitiari kama tamathali ya usemi ambayo hutumiwa

kulinganisha vitu viwili tofauti au vyenye tabia tofauti bila kutumiwa viungo vinavyotumiwa katika tashbihi.

Sitiari kuu ni aina ya sitiari ambayo hutawala kazi ya kifasihi, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Sitiari ya aina hii hurudiwarudiwa au kurejelewa na mtunzi kila mara na hujitokeza kuwa motifu. Jukumu la sitiari kuu ni kuwasilisha dhamira na maudhui katika kazi ya kifasihi.

Katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli,* sitiari kuu imetumika kwa wingi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utenzi wote. Mfano mzuri ni sitiari ya wanyama wawili ambao wamerejelewa kwa njia tofauti.  Wanyama hawa ni **kilabu** ambaye kwa jina la Kiswahili ni *mbwa.* Mnyama wa pili ambaye pia amerejelewa kwa wingi ni **simba**.  **Simba** pia amerejelewa kwa majina tofauti kama **asadi** au **usudi** kwa wingi.

Sitiari ya **kilabu** au **mbwa** imesheheni karibu utenzi wote kama vile tulivyodhihirisha. Neno hili **kilabu** limetumiwa na Waislamu kuwarejelea maadui wao ambao ni makafiri. Katika dini ya Waislamu **mbwa** ni mnyama haramu.  Kwao **mbwa** ni mnyama aliyelaaniwa na ambaye hastahili heshima kwa vyovyote vile.  Kule kuwafananisha makafiri na **mbwa** ni sawa na kuwatusi na kuonyesha vile wanavyowachukia. Pia ni madharau ya hali ya juu.

Kwa upande mwingine, pia yaweza kuwa ni ishara kwamba, mtunzi wa utenzi huu alikuwa akionyesha hisia zake wazi wazi juu ya msimamo wake kwa makafiri na Miungu yao ya sanamu.  Hii ni kwa sababu anawaita **kafiri** yaani watu wasio na dini.

Hata hivyo katika jamii nyingi, **mbwa** ni mnyama ambaye haheshimiwi na huchukuliwa kama mnyama asiyestahili heshima. Aina hii ya sitiari kwa kawaida ni **sitiari chakavu** kwani inachukuliwa tu kama neno la kawaida na sana sana kama matusi. Mtu anapofananishwa na mbwa huwa ameshushwa hadhi na hivyo kukosa heshima kwa wanajamii husika. Kwa sababu ya kutumika sana kwa wingi katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* sitiari hii ya **mbwa** tumeichukulia kuwa sitiari kuu kama vile tumedhihirisha katika maelezo yetu. Kwa mfano katika ubeti ufuatao:

Takupa tena Habibu
Jina ya huyu **kilabu**
jinale itwa shahabu
au mtu mashuhuri
(ubt[1] 79)

Mtunzi anamwelezea juu ya kiongozi wa makafiri ambaye ni **Rasi'lGhuli.** Kwa kumrejelea kisitiari kama **mbwa** jina lake kamili ni *Shahabu*. Anamweleza Tumwa wake kuwa ni mtu mashuhuri. Kwa kutanguliza kumwita **kilabu** anamaanisha ni mtu ovyo kama **mbwa** hata kama ni mashuhuri. Hii ni sitiari ya kumdunisha na kumfanya kuonekana mtu asiyestahili heshima. Mtunzi anaendelea kusema kuwa anatawala **kilabu** asiyemjua Mungu. Ana ujeuri mwingi na madharau.Kwa mfano:

1

Akitawala **kilabu**.

asijue wake Rabu

akashika kughusubu

kwa jeuri kukithiri

(ubt.84).

Hii ina maana kwamba makafiri wanaongozwa na kiongozi asiyemcha Mungu wala kumheshimu. Kutokuwa na dini ni sawa na **mbwa** ambaye kwa kawaida huwa hajui kama kuna Mungu wala dini na ndipo **Rasi'lGhuli** anafananishwa na **mbwa**.

Katika ubeti wa 275, imedhihirika wazi kwamba siye *Rasi'lGhul*i pekee aliyekuwa akiitwa **kilabu** au **mbwa** bali ni makafiri wote. Mtunzi anaelezea jinsi maluuni mmoja alipoingia nyumbani kwa sultani na kumwua. Baadaye akakalia kiti chake na kuvaa taji yake. Ghulamu alipoingia akamtuma kumwita Ali. Naye Ali hakukawia alifika na upanga mkononi. Yule maluuni kumwona Ali, akaamka kwa haraka akitaka kumpiga kwa ujeuri wake. Mtunzi anamrejelea maluuni huyo kama **kilabu** anasema:

Waziri kitaqarabu

akaajili **kilabu**

akema kumdhurubu

kwa ile yake jeuri

(ubt.275.)

Hata hivyo katika ubeti unaofuata, Waziri aliweza kumkata kwa dhoruba moja akaanguka vipande viwili. Kila mara mtunzi anataka kuonyesha ushindi kwa Waislamu dhidi ya makafiri ambao wana wadharau sana. Hii ndio sababu kila mara wanawadunisha makafiri

kwa kuwaita **kilabu**. Jambo hili linawafanya kuonekana wasio na uwezo wa kumshinda adui yao ambaye ana Mungu wa kumsaidia.

Ubeti mwingine unaodhihirisha kwamba **kilabu** ni jina lililowarejelea makafiri wote ni wa 287. Mtunzi anaelezea jinsi askari wa makafiri walipowavaamia Waislamu. Kiongozi wa makafiri aliwaelezea kwa kuapa kwa jina la Mungu wao kuwa atawapiga na kuwatendea vitendo vibaya na baadaye awachinje kama **ngamia**. Nao Waislamu wakamjibu yule **kilabu** kwamba wameyasikia maneno yake yote na wataenda kumweleza sultani wao. Kule kumrejelea kiongozi wa makafiri kama **kilabu** ni dhihirisho tosha kuwa sitiari hii ya **kilabu** haikuwa inamrejelea **Rasi'lGhuli** pekee bali makafiri wote kama walivyowaita Waislamu.

Sitiari hii ya **kilabu** pia inathibitisha kwamba makafiri walikuwa wa kiabudu sanamu. Na labda hii ndio sababu walikosa heshima kwa Waislamu na kuwafanya wawaite **kilabu** au **mbwa**. Kwa mfano, mtunzi anasema:

Yule kufari kidhabu
**sanamu** kafanya **Rabu**
akiabudu **kilabu**
daima kula shahari
(ubt 334)

Mtunzi anamrejelea **Rasi'lGhuli** kama **kafiri** mwongo aliyefanya **sanamu** kuwa Mungu wake. Anamfananisha na **mbwa,** kwani anaiabudu hiyo **sanamu** kila mwezi. Sitiari hii ya **kilabu** ambayo ni mfano wa **sitiari chakavu** inamaanisha kwamba, ikiwa mtu hakubaliani na imani ya Waislamu, basi huyo ni sawa na **kilabu** au **mbwa**. Hii ni kwa

sababu wale wote ambao walisilimu hawakuitwa **kilabu** tena, bali walichukuliwa kama mmoja wao. Kwa mfano. Arijifu alipokiri na kusilimu alikubaliwa kama mmoja wao

Nimeona tahaqiqi
ya dini kuwa haqiqi
nawe tumwa msadiqi
na **shahada nimeqiri**
(ubt.2262.)

Haya ni maneno ya Arijifu, baada ya kukubali kusilimu na kufuata dini ya Waislamu. Mwingine aliyesilimu na kuachwa kuitwa **kilabu** ni **Muqaliqali,** mwanaye **Rasi'lGhuli.** Alishauriwa na nduguye Arijifu kusilimu, lakini kwanza alimuumiza kwa kumkata kwa upanga. Baadaye alijuta na kuja kumtembelea Arijifu katika hema lake alipokuwa anauguza majeraha yake. Arijifu alidhani alikuwa amekuja kumwua na ndipo Muqaliqali akamwambia maneno haya

Siniue nduu yangu
nimerudi roho yangu
ya **kumtii Muungu**
pamwe na Tumwa Bashiri.

Nimejua tahaquqi
**dini** hii kuwa hadi
kwa leo **nimesadiqi**
nimetakasa dhamiri.
(ubt.3068-3069)

Baada ya kukiri na kukubali kusilimu, **makafiri** walikubaliwa na kuachwa kutambuliwa kama **kilabu**. Kwa maoni yetu ni kwamba sitiari hii ilikuwa ikiwarejelea wale ambao hawana imani ya kiislamu au wale ambao hawaamini mambo ya Mungu na mtume wake Muhammadi hata kama ni Waarabu.

**Sitiari ya kilabu** imesheheni katika utenzi wote na kuifanya kuwa **sitiari kuu** ingawa kwa kawaida ni **sitiari chakavu** au **fifi**. Mifano mingine ya beti ambapo sitiari ya **kilabu** imetajwa ni kama vile 472, 503, 540, 794, 869, 891, 980, 984, 1063, 1076, 1174, 1246, 1259, 1290, 1329, 1387, 1423, 1428, 1507, 1538, 1543, 1568, 1653, 1718, 1740, 1775, 1792, 1835, 1871, 1981, 2036, 2040, 2045, 2105, 2136, 3381, 3412, 3532, 3554, 3599, 3680, 3693, 3730, 3744, 3818, 3532, 3554, 3599, 3680, 3693, 3730, 3744, 3818, 3824, 3848, 3903, 3938, 3946 na 4529. Kwa ufupi neno **kilabu** imerejelewa zaidi ya mara tisini na tatu katika utenzi wote. Na kwa sababu imetumika kama sitiari ikawa kiamba jengo cha kuyaendeleza na kuyakamilisha maudhui ya mtunzi pamoja na kuikuza dhamira yake na kuwatambulisha wahusika wa upande wa makafiri pamoja na kuelezea zaidi sifa zao, matendo yao na sababu za kushindwa kwao na Waislamu. Pia kwa maoni yetu, sitiari hii imedhihirisha wazi wazi mtu asiyemwamini Mungu ni sawa na **kilabu** kwani daima atashindwa katika mipango yake.

Kulingana na imani hii ya Waislamu, kumwabudu Mungu na kuamini mtume wake Muhammadi na mafundisho ya Quran tukufu kuna mtofautisha binadamu na **mbwa** au mnyama ambaye ni mpotofu na asiyeheshimiwa. Kumaanisha kumjua Mungu kunamfanya binadamu kuwa mstaarabu, muungwana na wa kuheshimiwa.

Aina nyingine ya sitiari kuu katika **Utenzi wa Rasi'lGhuli** ni sitiari ya mnyama **simba.** Sitiari hii inapatikana katika beti nyingi. Kwa kawaida **simba** hujulikana kama mnyama hodari, mwenye nguvu, asiye na woga, jasiri na anayeogopwa na kila mnyama, hata binadamu. Dyer (1973) anawataja simba, chui na nyati kuwa miongoni mwa wanyama watano ambao ni wenye nguvu na wanao ogopwa zaidi na binadamu na pia wanyama wenzao.

Kulingana na mtunzi wa utenzi huu, **simba** ni sitiari ya ushupavu na ujasiri. Viongozi wa pande zote mbili wametumia sitiari hii ya **simba** ili kudhihirisha ujasiri wao katika vita. Katika utenzi huu **simba** pia ametambuliwa kwa majina kama **asadi** na pia **usudi** kwa wingi. Majina haya yote yanamrejelea mnyama mmoja ,yaani **simba.** Kwa kawaida **simba** huwa ni hodari na shupavu kwa kuwinda na kuua windo lao. Ni kutokana na sifa hii ambapo majeshi hupenda kujitia nguvu kwa kujifananisha na **simba** wanapoenda kupigana vita na kuwaua maadui wao.

Aina hii ya kulinganisha mtu na **simba** ni mfano wa **sitiari sahili.** Hii ni kwa sababu sitiari hii huwa nyepesi na rahisi kueleweka na hadhira. Ulinganisho wake ni wa moja kwa moja. Hata hivyo, kwa kuwa sitiari hii ya **simba** imetumika kwa wingi katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* tumeichukulia kama **sitiari kuu**. Kwa kawaida aina nyingi za sitiari huwa na ugiligili mwingi na hubidi kutofautishwa kulingana na mukhtadha wake.
Tabia za viongozi wa majeshi kujitambulisha kama **simba** zimejitokeza kwa wingi katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Kwa mfano;

Naye kijana tuwili
yukinga **simba** mkali
na sura yake jamali
na wajihi mduwari
(ubt.754.)

Mtunzi hapa anaelezea jinsi kijana wa makafiri alivyotokea bila wao kutarajia akiwa na sura ya **ngamia** na kufanana na **simba** mkali na uso wa ujasiri. Mtunzi ametumia nafsi ya tatu kuelezea hali ilivyokuwa wakati huo kijana alipotokezea Ali na Sahaba wake. Sitiari hii inadhihirisha weledi, ushujaa na ujasiri aliokuwa nao huyo kijana. Mpaka Ali akawashauri masahaba wake wasimshambulie wakati huo kwani aliona hali ya huyo kijana ikiwa ya kutisha. Kwa upande mwingine, inaweza kuwa ni mbinu ya kuwasawiri Waislamu kuwa werevu kuliko makafiri. Hii ni kwa sababu Ali kiongozi wa masahaba alipoona jinsi huyo kijana alivyokuwa na ujasiri wa simba**,** aliwashauri kurudi nyuma.

Naona mna ajili
ya kuwania qutali
tunzeni kwanza dalili
**mambo yataka shauri**
(ubt.763.)

Na pia katika ubeti ufuatao anawaelezea masahaba wake wazi wazi kuwa nguvu za yule kijana ni bayana yaani wazi na ushujaa wake unadhihiri .

Nami hitunza naona

**nguvu zake mbayana**

ahimili na kuwana

ushujaa udhahiri

(ubt.764)

kwa maoni yetu, mtunzi alitumia sitiari hii ili kuonyesha kushinda vita si kwa kuwa jasiri na silaha kalikali bali ni kwa kutumia akili kama alivyofanya Ali. Kwa hivyo ni ushindi kwa Waislamu. Pia yaweza kuwa dhihirisho kwamba Mungu wao amewaongoza kufikia uamuzi huo ili kuepukana na maafa ambayo wangesababishiwa na huyo kafiri na wafuasi wake.

Katika ubeti wa 833, mtunzi pia anatumia sitiari ya **simba** ili kuonyesha ushujaa na ujasiri wa masahaba wake. Mmoja wao alitolewa juu ya **farasi** na kurushwa hadi kwenye kundi la askari wa makafiri. Hata hivyo, mtunzi anasema kuwa, akiwa kwenye kundi la askari aliwakatakata bila kurudi nyuma, na kusema kwamba alijikinga kama **simba** wa bara.

Hapa anamfananisha askari wake na **simba** wa bara ambao wanaaminika kuwa jasiri na hodari katika kupambana na adui wao au windo lao. Mtunzi hapa ametumia nafsi ya tatu ili kuelezea ushujaa wa askari wa Waislamu.

Hata hivyo kuna matumizi ya nafsi ya kwanza ambayo yametumiwa na viongozi wenyewe ili kujigamba kwa uwezo na ujasiri walio nao. Kwa kawaida usimulizi huu unatumika pale ambapo watu wawili wanazungumza ana kwa ana kwa njia ya dayolojia,

kujisifu au kudhalilisha adui wao. Ni njia moja ya kueneza propaganda ili kuwatia wapinzani wao woga. Mfano mzuri unapatikana katika ubeti ufuatao:

Ndimi **simba** maarufu
ndimi **mvunda sufufu**
wajapo kuwa alfu
siwajali sifikiri
(ubt.847)

Katika ubeti huu, Ali anajipigia debe na kupigia chuku umaarufu wake kwa kumweleza adui yake kuwa yeye ndiye simba maarufu na ndiye mwangamiza wengi, hata kama watakuja kwa maelfu hawajali na hawamsumbui. Aina hii ya sitiari pia hutumiwa ili mtu kujitia moyo na kuondoa woga ili apate nguvu za kupigana.

Sitiari nyingine ya aina hii katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*, inapatikana katika ubeti ufuatao:

Akiwamo kujisifu
ndimi **simba** maarufu
ndimi **mvunda sufufu**
wajapo kuwa kathiri
(ubt 866)

Tofauti ni kwamba maneno haya yanasemwa na **ghulamu** au mvulana kutoka upande wa makafiri ambaye ni askari akimweleza Imamu walipokutana ana kwa ana katika vita. Jambo hili laonyesha sitiari hii ya kujigamba na kujisifu kwa uwezo na ujasiri wa **simba** inatumiwa na pande zote mbili.

Katika ubeti wa 1435, 1489, 1582, 1806, 2464, 2818, 2819 na zingine, Ali ambaye anajulikana kama "Haidari" yaani **simba** jina la kimajazi anajigamba na kujisifu akifananisha uwezo wake na uwezo wa **simba.**

Mwingine ambaye ana mazoea ya kujigamba na kujisifu mbele ya maadui wake ni Umari bun Maad kwa jina la utani ni Safwati bin Ubadi. Tazama ubeti ufuatao:

Ndimi **simba** maarufu
ndimi **mvunda sufufu**
nishikapo yangu sefu
huwadhili makufari
(ubt 3367)

Anasema yeye ndiye **simba** maarufu ambaye anaangamiza wengi. Akishika upanga wake mrefu huwaangamiza makafiri. Kuna beti pia amerejelewa na sahaba wengine. Nazo ni 2088, 3368 na 2094. Rasi'lGhuli naye pia alitumia sitiari hii ya **simba** kuapa na kujisifu kwamba yeye ni hodari na jasiri kama **simba.**

Ndimi mwana abtali
walidi Rasil'Ghuli
ndi mimi **simba** mkali
ndimi shujaa jasuri
(ubt.2129.)

Hili ni thibitisho kwamba pande zote mbili zilikuwa zinatumia sitiari hii ya simba kujisifu na kuwatisha maadui wao. Ni mbinu ya kutia chumvi maneno ili yaonekane ya kweli. Pia nao watu wake walimrejelea kwa kumfananisha na **simba,** kwa mfano katika

ubeti wa 1576 na 1883. Wengine waliorejelewa na mtunzi mwenyewe ni kama Aba Hasani, Zuheri, Jendele, Waziri, Mwana kindi, Miqidadi na Ali . Walirejelewa katika beti zifuatazo 274, 656, 675, 743, 801, 837, 1555, 1820, 2140, 2305, 2553, 2530, 2144, 1805, 1773, 1868, 1492 na 3434.

Hata hivyo, kuna sitiari za **simba** ambazo wanajigamba kuwa shujaa wa Mungu yaani wanajisifu na nguvu za Mungu na sio zao wenyewe. Baadhi yao ni Shekhe Alia katika ubeti huu:

Ndimi **simba wa Mungu**
ndimi mkusa matungu
ndimi muwanya mafungu
ndimi mpangua ari
(ubt 1582)

Shekhe Ali anajiita **simba** wa Mungu ambaye anatawanya mafungu na kupangua mambo. Sitiari ya aina hii ina upole na hata kama anajisifu ni kwa njia isiyo ya wazi. Nia yake hapa ni kumwinua Mungu kuonekana ndiye anamsaidia kushinda vita.

Mwingine pia aliyefuata mtindo huo ni Zuheri Muwani. Anasema hivi katika ubeti ufuatao:

Ndimi Zuheri Muwani
ndimi **simba wa amani**
auladi Qahlani
qabila bin Amiri
(ubt 1805)

Zuheri anajitambulisha na kabila lake kwa kusema ndiye Zuheri Muwani **simba** wa amani mwana wa Qahlani kutoka kabila la Amiri. Sitiari ambayo ametumia ni kama kiapo si kujigamba na kujisifu kama wale wengine na pia ubeti wa 1567 Ali anawaita Waislamu **simba za Mungu**.

Sitiari ya **simba** imetumiwa na pande zote mbili kwa minajili ya kujisifu, kuonyesha uwezo wao na ujasiri wao kama **simba.** Sitiari hii imesaidia pakubwa katika kufanikisha kazi ya mtunzi kimtindo kwa sababu, ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza pale ambapo wahusika walikuwa wakijisifu mbele ya maadui wao. Pia ametumia nafsi ya tatu kuelezea baadhi ya wahusika na sifa zao. Hata sehemu zingine ametumia wahusika wake kuwaelezea sifa za wahusika wengine kama vile tumedhihirisha.

Kupitia kwa sitiari hii ya **simba,** pia dhamira ya mtunzi imeweza kukuzwa zaidi. Maudhui pia yamejitokeza kwa wazi kupitia sifa za wahusika hawa katika mbinu hii ya sitiari ya **simba.** Kimtindo pia mtunzi aliweza kufanikisha kazi yake kwa ujumla. Ikiwepo ni kuchagua maneno ambayo yangesawazisha mizani na vina. Kwa maoni yetu sitiari hii imefanikisha kazi ya mtunzi kifani.

Neno “kufari” pia limetumika kama aina ya **sitiari sahili.** Na kwa kuwa imetumika kwa wingi sana katika *utenzi Rasi’lGhuli* tumeitambua kama **sitiari kuu.** “Kufari” maana yake ni kafiri yaani mtu asiye na dini au asiyemwamini Mungu wa kweli. Neno hili limetumiwa sana kuwarejelea makafiri ambao Waislamu wanaamini wanaabudu sanamu. Sitiari hii ya kufari imetumika zaidi ya mara mia mbili. Limetumika mara moja katika beti zaidi ya mia mbili. Ni ubeti mmoja tu limetumika mara mbili. Kwa hivyo linastahili kuwekwa katika kundi la **sitiari kuu.** Sitiari hii ya “kufari” imetumiwa kwa mara ya

kwanza katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* na Wafari binti Sadamu. Katika ubeti ufuatao anasema:

Nisikilize Tumwa wetu
huko janibu ya kwetu
kuna khabithi ya watu
sultani wa **kufari**
(ubt 78)

Wafari anamweleza Tumwa wao kuwa asikilize kwa makini kwamba kule upande wa kwao kuna watu wabaya na wachafu na sultani wao ni kafiri. Ametumia neno **kufari** kisitiari kurejelea watu wa kwao ambao hawana dini. Inaonekana alikuwa ametoka huko kwa Rasi'lGhuli kwani tunaambiwa ni wa kabila la Rubui.

Neno hili laweza kuchukuliwa la kawaida lakini likitazamwa kwa makini limetumika kama sitiari sahili ambayo imezoelewa katika jamii na kuonekana la kawaida. Kwa upande wetu neno hili ni sitiari hasa na tumelitazama katika mukhtadha huo.

**Sitiari** hii ya "kufari" haikutumiwa kumrejelea tu sultani wao ambaye ni Rasi'lGhuli, bali na hata watu wote ambao wanaaminika na Waislamu kutokuwa na dini wala kuamini Mungu wa kweli. Kwa mfano katika ubeti huu mtunzi ameandika:

**Kufari** wakikutana
mjini wakingizana
kukawa kiza mtana
kwa junudi kukithiri
(ubt 299)

Mtunzi anaeleza vile makafiri wakiingia mjini kunakuwa giza mchana kwa sababu ya askari kujaa. Hii ni thibitisho kwamba sitiari hii ya **kufari** haimrejelei sultani wao pekee bali hata makafiri wote. Beti zinazomrejelea sultani wao **Rasi'lGhuli** kama **kufari** ni 359, 364, 383, 395, 423, 424, 4182 na 4317 .

Sitiari **kufari** pia imetumika kuwarejelea makundi tofauti tofauti katika beti tofauti tofauti. Kwa mfano **askari,** nchi ya **kufari**, wana wa **kufari** au **makufari**. Beti hizi ni nyingi na tutatoa baadhi tu 423, 424, 429, 613, 629, 673, 712, 747, 823, 1462, 1501, 1505, 1525, 1562, 1636, 1660, 1654, 1675, 1686, 1712, 1713, 1750, 1760, 1771, 1794, 1813, 1830, 1832, 1882, 1897, 1903, 1911, 2024, 2039, 2055, 2062, 2066, 2074, 2106, 2140, 2165, 2168, 2185, 2193, 2204, 2280, 2315, 2283, 2315, 2334, 2391, 2433, 2440, 2517, 2522, 2536, 2605, 2610, 2636, 2721, 2735, 3834, 3861, 3867, 3888, 3913, 3957, 3990, 4025, 4049, 4132, 4247, 4294, 4308, 4317, 4469, 4504, 4507, 4520, 4542 na 4565.
Kama nilivyotangulia kusema beti zote ni zaidi ya mia mbili na nimetaja tu baadhi bila kufuata mpangilio wowote. Sitiari hii ya **kufari** imetumika kwa kuanzia sentensi, katikati mwa sentensi au mwishoni mwa sentensi bila mpangilio maalum. Ubeti huu ni tofauti;

Akiwapiga kwa panga
**kufari** wakimzinga
zuberi wakimfunga
wakifurahi **kufari**
(ubt 498)

Katika ubeti huu neno **kufari** limetumiwa **mara mbili** kwa ubeti mmoja, labda katika kusisitiza ushindi wa makafiri ambao hautadumu, kwa sababu Zuberi atakuja kutoroka. Na pia labda mtunzi kuonyesha ujuzi alionao wa kutunga shairi.

Ubeti mwingine ambao pia ni tofauti na zingine ni ubeti ufuatao;

Usiku kupambazuka
walitoza mushirika
wawene watu kanguka
**qaumu ya makufari**
(ubt 1780).

Ubeti huu ni wa kipekee kwani mtunzi ametumia msemo kuwasilisha ujumbe wake. Hii ni aina ya sitiari ambayo hutumia misemo na nahau ili kulinganisha. Sitiari hii ndiyo tulielezea katika sura ya pili kama **sitiari chakavu.** Ubeti wa mwisho ambao pia tunaona ni muhimu kunukuu ni ubeti ufuatao;

Akiwambia Imamu
tini mola karimu
wadiridhi kusilimu
**hata wahindi kufari**
(ubt 1788).

Ubeti huu ni muhimu kwani ni thibitisho kamili kwamba mtu yeyote ambaye hakubaliana na imani ya Waislamu kwao ni kafiri kama vile wanavyowarejelea **Wahindi** katika ubeti huo.

Ni muhimu kutaja hapa, kwa maoni yetu, neno **kufari** laweza hata kuwarejelea Waarabu kwani kila watu huwa na Mungu wao ambao wanamwabudu na wanaamini huwasikiliza na kuwatimizia haja zao.

### 3.1.1 Sitiari sahili

Aina hii ya sitiari huwa nyepesi na rahisi kueleweka na hadhira.Hii ni kwa sababu ulinganishi wake ni wa moja kwa moja hasa,katika mukhtadha wa kivita kama katika utenzi huu.Kuna mwingiliano mwingi baina ya aina hizi za sitiari,kwa hivyo itatengemea matumizi yake katika mukhtadha, Katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* aina hii ya sitiari imetumika kurejelea baadhi ya aina za wanyama. Ndege nao pia wametumika aidha kwa sababu ya ukali wao au mbio zao. Vifaa au vyombo pia vimetumika kuthihirisha hali ya mambo katika sehemu husika. Vilevile viumbe dhahania kama jinni, jitu na shetani vimetumika kama vile tumedhihirisha.

Kuna baadhi ya ndege waliotumika kisitiari katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Kwa mfano, **kozi**, **mwewe** na **tai** pia anajulikana kama **Iqabu** kwa kiarabu.

Ndege hawa watatu ni hatari sana katika kuwinda wana kucha kali na mdomo unaoweza kumrarua adui vibaya sana. Pia wana uwezo wa kupaa juu sana angani na kuteremka kwa mwendo wa kasi sana. Ndege hawa wana uwezo mkubwa wa kuona mbali na hata vitu vidogo sana wakiwa juu sana angani. Ni kwa sababu ya sifa hizi ndipo viongozi na askari pamoja na sahaba katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* wanajifananisha nao kisitiari.

Katika ubeti ufuatao mtunzi anaeleza jinsi Rasi'lGhuli alivyotawala baada ya kifo cha babake na kuendeleza ufidhuli.

Akitawala mwanawe

**akinga Kozi na Mwewe**

ya mola asiyajue

akazidi kukufari

(ubt.83)

Mtunzi anaelezea kuwa baada ya Rasi'lGhuli kutawala alijikinga kutokana na **kozi** na **mwewe** ambao ni adui wake makafiri bila kujua ya Mungu na akaendeleza mambo ya ukafiri. **Kozi** na **mwewe** hapa wanawarejelea sahaba na majeshi ya Waislamu. Wanajifananisha na uwezo wa **kozi** na **mwewe** wa kuweza kutambua lilipo windo lao na kuliangamiza.Sababu za kuwaweka katika kikundi cha sitiari sahili ni kuwa hawajitokezi kwa wingi katika utenzi na ni rahisi kueleweka.

Beti zingine zinazorejelea uwezo wa ndege hawa ni 700, 908, 1228, 1329, na 1647. Kuna baadhi ya beti ambazo zimetumia sitiari ya ndege yaani **nyuni** au **tuyuri** bila kutofautisha ni ndege wa aina gani. Sitiari hii ya **nyuni** imetumika kuonyesha uwezo wa kwenda haraka au kufanya mambo kwa haraka kama vile **nyuni** wanavyofanya. Sahaba na askari wao walikuwa wakifanya kazi kwa haraka mno. Kwa mfano, kupanda kwa farasi,kukimbia, kuangamiza adui wao kwa muda mfupi na kadhalika. Katika ubeti ufuatao ni ithibati tosha ya aina hii ya sitiari.

Nikiruka kama **nyuni**
nikipanda farasini
kwa nyuma ya muongoni
nikimwandika khanjari
(ubt.1411.)

Ali anaelezea jinsi alivyopanda farasi wake kwa haraka kama **nyuni,** kuonyesha wepesi na uwezo wa kufanya mambo kwa urahisi. Pia katika ubeti huu anasema.

Alipokwisha kwanguka
name ni wele kupoka
kana **nyuni** ni kuruka
hizama katika bari
(ubt 1412)

Ali anaendelea kueleza uwezo wake katika vita. Anasema baada ya adui wake kuanguka anakimbia kama vile **nyuni** wanavyoruka na kuzama katika bara. **Nyuni** hapa inatumika kama **sitiari sahili** kwa sababu anajifananisha na **nyuni** katika kutenda mambo kwa wepesi na kwenda mbali sana kwa muda mfupi.Ni ulinganisho wa moja kwa moja. Beti zingine zenye sitiari hii ya **nyuni** ni kama 358, 699, 700, 732 na 1394.

Kuna baadhi ya wanyama ambao pia wametumika kama **sitiari sahili**. Wanyama hawa ni kama **nyati, majoka** na **chui** ambaye pia anaitwa **namiri.** Wanyama hawa ni hatari sana. Kwa mfano, **nyati** akishambulia adui yake hutumia miguu, meno, kichwa na hata makojoo yake ili kumwangamiza adui wake.

Naye **nyoka** ana sumu hatari ambayo inaweza kumwangamiza adui wake mara moja. Wengine kama **chatu** wana uwezo wa kumeza adui wake baada ya kumvunjavunja mifupa yake. **Chui** naye ni mnyama hatari sana. Anatumia meno na kucha zake kupambana na adui wake na haogopi chochote. Kwa kujifananisha na wanyama hawa kisitiari ni njia ya kuonyesha uhodari walionao dhidi ya maadui wao na jinsi wanaweza kuwaangamiza kwa urahisi.

Kwa mfano:

Akija tena wa tatu
yukinga **nyati wa mwitu**
akinadi mara tatu
pale alipo zuheri
(ubt.1959.)

Mtunzi anaelezea uwezo wa Zuheri ambaye ni Muislamu wa kupambana na adui wake. Anaelezewa vile alijikinga kama **nyati wa mwitu** na kuwaangamiza adui wake. Neno **nyati** limetumika kisitiari kuonyesha Zuheri alikuwa na sifa za **nyati** kama nilivyoeleza hapo juu. Beti zingine zilizorejelea sitiari ya mnyama **nyati** ambaye pia anatajwa kama **ng'ombe wa mwitu** ni 1832 na 2586. **Chui** na **nyoka** wametumiwa kisitiari kurejelea vile mazingira yalivyokuwa huko **nyikani** walikokuwa wakipigania pia **nyoka** anatumiwa kumrejelea adui yao Waislamu ambao ni makafiri. Wanafananishwa na **nyoka** kwa sababu wanaweza kuwaua kwa haraka kama vile sumu ya **nyoka** hufanya. Vile vile kulingana na Waislamu **nyoka** amelaaniwa kulingana na Quran Tukufu. Kwa hivyo hawa makafiri kwao ni wajalaana. Ubeti ufuatao unathibitisha haya:

Wangwana alipofika
ndiaze zina mashaka
**mna simba na majoka**
na majini na namiri
(ubt 585)

Mtunzi anaelezea vile mazingira yalivyokuwa huko jangwani. Kwa kutumia sitiari za simba, majoka**,** majini na namiri ambaye ni chui. Wanyama hawa wote pamoja na majitu ni hatari kwa hivyo anajaribu kutuchorea picha jinsi huko nyikani kulikuwa na hatari nyingi. Hata njia ambazo walipitia zilikuwa na mashaka mengi. Mtunzi ametumia mbinu ya kinaya pamoja na chuku kuelezea hali ilivyo kuwa. Ni kinaya kwa sababu sio rahisi kupata simba na chui jangwani. Pia amejumuisha wanyama pamoja na majini kwa njia ya chuku ili kusisitiza shida zilizokuwepo. Ametumia mbinu ya taswira ili tuelewe mandhari ya hatari zilizokuwepo huko jangwani. Mbinu hizi zote zinachangiana ili kufanikisha kazi ya mtunzi kifani.

Ubeti ufuatao ni mfano wa vile Waislamu wanavyowarejelea makafiri kama **nyoka.**

Nami nataka unende
na **nyoka** ukamtinde
umuwanye pande pande
na mimi nikubusuri
(ubt.649)

Katika ubeti huu mtunzi ametumia sitiari ya **nyoka** kuwarejelea makafiri. Ali anatumwa aende kumchinja huyo **nyoka** na kumgawanya vipande vipande. Kuna beti zingine kama 645, 648, 585, na 932 ambazo pia sitiari ya **nyoka.** Imetumika kuwarejelea makafiri kama walaaniwa kama **nyoka**.

Kuna wanyama **wapole** pia waliotumika kisitiari katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Wanyama hawa ni kama vile **ngamia**, **kondoo, farasi** na **mbuzi**. **Ngamia** ametumiwa ili kuonyesha mbinu za usafiri huko jangwani. **Ngamia** ana uwezo wa kwenda siku nyingi bila kunywa maji na hata chakula. Ana uwezo wa kuvumilia maisha magumu. Kwato zake zinaweza kuvumilia miiba, mawe na kutembea kwa urahisi kwa changarawe.

Beti ambazo zinamrejelea **ngamia** ambaye pia anaitwa **jamali** na tena **bairi** ni kama vile; 52, 286, 388, 438, 542, 767, 948, 1003, 1010, 1029, 1031, 1057, 1090, 1523, 4382 na 4391. **Farasi** pia ametumiwa kisitiari kutokana na uwezo wake wa kukimbia mbio sana na kutokuwa na woga. Pande zote mbili yaani Waislamu na makafiri walitumia **farasi** wakati wa kupigana mara nyingi. Hii ni dhihirisho kwamba **farasi** anaweza kutumika kumwokoa mtu kwa kumwondoa kutoka kwenye eneo la hatari. Pia anaweza kutumika kumkimbiza adui. Kwa mfano;

Wakitokea kwa **kasi**
shabihi rihi ya kusi
na kivumi cha **farasi**
kana mwamba wa bahari

(ubt.1800)

Mtunzi anaelezea jinsi **farasi** walikuwa wakitumika kwa kwenda mbio kama upepo wa kusini na sauti ya **farasi** wakikimbia wakiwa imara kama mwamba wa bahari. Beti zilizoandikwa kurejelea sitiari hii ya **farasi** ambaye pia anaitwa **khuyuli** ni kama,1523, 1800, 2170, 2179, 2374, 2454, 2459, 2496, 2560, 2612, 2638, 2639, 2647, 2734, 2751, 2754, 2761, 2841, 2908, 3299, 3250, 3356, 3378, 3432, 3448, 3719, 3767, 4056, 4057, 4073, 4296 na 4299 .

**Kondoo** ametumiwa kisitiari kama njia ya kumtolea Mungu kafara na pia kama ishara ya chakula. Kisitiari **kondoo** ni mpole na ni ishara ya amani. Katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* mnyama huyu ametumiwa kama ifuatavyo;

Katika safari yao
wametukua **kondoo**
akitwaa bwana wao
kutinda asiqasiri

(ubt.768).

Mtunzi anaelezea jinsi sahaba walivyochinja **kondoo** wakatoa ngozi yake halafu wakala. Baada ya kula tunaelezewa walipata nguvu na Tumwa wao akatumwa kuleta habari. **Kondoo** pia ametajwa kisitiari katika beti zifuatazo 774 na 775.

**Wadudu** nao pia walitajwa kisitiari katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Kwa mfano **nyuki**. Mtunzi ametumia sitiari ya **nyuki** ili kuonyesha uwezo wa Mungu dhidi ya makafiri.

Achenda kuwabusuru
na **nyuki** wasimdhuru
na mola kuwaumuru
kumtii Haidari
(ubt.2969.)

Mtunzi anaeleza jinsi **nyuki** walivyoamrishwa na Mungu kumtii Ali ambaye pia anaitwa Haidari na wasimdhuru. Katika ubeti unaofuatia anaeleza vile nyuki walimfuata Haidari na kuwafukuza kufari. Beti zingine ni 2968 na 2970. Ni sitiari ambayo inaonyesha kuwa mambo yote yawezekana kama **nyuki** wanaweza kutumiwa kama silaha kusaidia kupambana na adui. Hata hivyo, tangu zamani kabla ya Waislamu kuingia Arabia. Waarabu wa Bedouin walihusisha tabia za wanyama na watu. Nyuki anafananishwa na Waislamu kwa sababu wanaishi na kufa wakifuata na kutii 'sharia' ambayo waliachiwa na Mungu.

### 3.1.2 Sitiari chakavu

Abrahams (1957:64) anaeleza kuwa **sitiari chakavu** imetumiwa sana katika lugha kwa kiasi cha kuifanya kuonekana kama si sitiari tena. Sitiari za aina hii huwa zimefungamana sana na matumizi ya kawaida ya lugha na hivyo kupoteza ubunifu wake. Mifano mizuri ya sitiari za aina hii inapatikana katika misemo na nahau. Katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* sitiari hii imetumika.

**Mshabaha wa tausi**

mzuri hana qiasi

amejipamba libasi

nguo njema za Hariri

(ubt.759.)

Katika ubeti huu mtunzi ametumia msemo ili kuelezea uzuri wa mwanamke ambaye alikuwa kama **tausi.** Kwa kawaida **tausi** huwa anapendeza na hivyo huringa kwa uzuri wake. Kule kumfananisha mwanamke huyu na **tausi** ni sitiari ambayo imepigiwa chuku. Aina nyingine ya **sitiari chakavu** katika utenzi huu inapatikana katika ubeti huu:

Usiku kupambazuka

walitoza mushirika

wawene watu kanguka

**qaumu ya makufari**

(ubt.1780.)

Mtunzi ametumia sitiari kwa njia ya msemo ili kuonyesha jinsi makufari walipouawa kwa wingi. Anaelezea kwamba kulipopambazuka walikuta kaumu ya makufari yaani watu wengi wakiwa wameuawa. Sitiari ya aina hii ni **chakavu** kwa sababu ya matumizi ya misemo na nahau ili kulinganisha au kufananisha.

Ni vizuri ieleweke kwamba sitiari hizi zina mwingiliano mwingi na mara nyingi hutegemea maoni ya mtunzi au mchambuzi na si lazima kukubaliana mahali pa kuweka mpaka baina ya sitiari hizi.

### 3.1.3 Sitiari Hisimseto

Aina hii ya sitiari hutumika kuhamisha hisia za kitu kimoja kwa kitu kingine. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*, majini, jitu, na **G**huli yametumiwa. Hawa ni viumbe dhahania na wanaweza kuleta athari za kihisia kwa sababu mara nyingi hawaonekani lakini vitendo vyao vyaonekana. Pia yanaweza kuwa na athari kwa mtu mmoja na mwingine hakuna. Neno Ghuli katika utenzi huu limetumika kama anayetokea katika maumbo mengi mbalimbali. Anawapoteza wasafiri na kuwameza akianza kutafuna mguu. Haya ni maelezo katika sehemu ya msamiati. Kwa hivyo kwa maoni yetu tunaweza kumchukuilia kama jini au jitu. Kwa mfano katika ubeti ufuatao:

Ndia awene thaqili
kwa **majini** na **maghuli**
kwenenda asihimili
awene kuwa khatari
(ubt 594).

Mtunzi ametumia majini na maghuli kuonyesha vile njia hiyo ilijaa hatari nyingi. Majini na maghuli yanaleta dhana ya hisimseto kwa sababu yameelezwa kuwa maghuli haya yanaweza kujibadilisha na kuchukua umbo lolote.Nayo majini kwa kawaida ni kama upepo na pia yana uwezo wa kujibadilisha na kuchukua umbo lolote. Hali hii ya kutojulikana yatajitokeza katika umbo lipi linaleta hisia tofauti kwa viongozi, sahaba na majeshi yao, hivyo ni hatari sana. Majini, maghuli na pia shetani yamerejelewa katika beti zifuatazo 635, 640, 642, na 667.

Wakati mwingine waislamu walikuwa wanawarejelea makafiri kama Ghuli. Kwa mfano ubeti wa 635. Pia kiongozi wa makafiri alikuwa akiitwa Rasi'lGhuli kumaanisha **kichwa cha nyoka.** Majina yote mabaya yalikuwa yanawarejelea makafiri. Mengi yao yalitumiwa kisitiari labda kwa sababu ya kuondoa ukali wa matusi hayo.

Tena kwa maoni yetu, ni kupunguza uzito wa maneno hayo na kujaribu kuleta upole kwa wasomaji ambao si Waislamu. Aina nyingine ya siitari hisimseto ni sitiari inayorejelea **jabari.** Neno jabari kulingana na maelezo katika sehemu ya msamiati ya *Utenzi wa Rasi'lGhuli*, linamaanisha mwenye nguvu au mwenyezi. Sitiari hii imetumika kurejelea nguvu za Mungu zisizo na kifani. Sababu ya kuweka neno **jabari** katika kundi la sitiari hisimseto ni kwa sababu nguvu ni za kihisia zinasikika au kudhihirika wala hazionekani. Pili wakati mwingine neno hili linatumika kuonyesha uwezo wa binadamu. Kwa mfano limetumika kumrejelea Ali na pia uwezo wa makufari. Matumizi haya yanalifanya kuwa **sitiari sahili.** Kwa hivyo, badala ya kulirudia tumeliweka katika kundi la **sitiari hisimseto.** Kwa mfano;

Mkuu wao wawene
ali yeye maluuni
aruwa wa safwani
ali anidi **jabari**
(ubt.1879).

Neno **jabari** hapa linamrejelea Aruwa wa Safwani ambaye ni mmoja wa viongozi wa makafiri. Mtunzi anamwelezea kama mkaidi asiyejua nguvu za Mungu pia mfano mwingine unaorejelea nguvu za makafiri unapatikana katika ubeti ufuatao:

Akitazama Amini
**jabari** za Maleuni
achondoka hiyo hini
akihimu askari
(ubt. 2599).

Beti ambazo zinarejelea nguvu za watu ni 1879, 2566, 2584, 2599, 2996 na 3384. Kuna beti pia ambazo zinarejelea nguvu za mwenyezi Mungu moja kwa moja kwa mfano:

Janadili akitunza
awene kumpendeza
moyoni akieleza
kutii mola **jabari**
(ubt.3477.)

Ubeti huu unataja nguvu za Mungu moja kwa moja. Katika mshororo wa mwisho anaeleza juu ya kutii nguvu za Mungu moyoni. Beti zingine ni kama 2858, 2930, 3356, 3727, 382, 3096, 2322, 2243, 2212, 2045 na 2005.

Matumizi ya aina hii ya sitiari ni ya kidhahania kwa sababu zile zinaitwa nguvu za Mungu huenda zikawa kwa wengine ni matukio ya kawaida.

### 3.1.4 Sitiari ya usuli

Sitiari za aina hii zinapatikana katika lugha nyingi ulimwenguni. Wamitila (2008:423) anaelezea kuwa sitiari ya usuli ni "….sitiari ambayo imefungamanishwa na lugha kiasi kwamba watu au wazungumzaji na watumiaji wa lugha hawaiangalii tena kama sitiari au

hawafikirii tena kama ni sitiari." Naye Mutiso (1996:123) anaelezea kuwa kawaida 'giza' linahusishwa na uoga, kushindwa, upweke, msiba, mashetani, mizuka, wanyama wala watu, uchawi, ujinga, miongoni mwa mambo mengine hasi. Kwa upande mwingine moto unahusishwa na hatari na maangamizo, nayo baridi inahusishwa na upweke na ukosefu wa furaha.

Kuna mifano mingi katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* ambayo ni ya aina hii. Baadhi ya vitu asilia ambavyo vimetumika kisitiari ni kama **nyika, jabali, pango**, **pepo** au **peponi bara, bahari, nuru, kiza, motoni, milimani, nyota, mtoni**, **Rihi ya kusi, mwezi** na **shajari (mti).**

**Nyika** imetumiwa kisitiari kuonyesha mahali ambapo vita vilikuwa vinatokea. Mtunzi anatumia sitiari hii kuonyesha ugumu na matatizo ambayo majeshi yote yanakubana nayo katika kutetea haki zao. Baadhi ya matatizo wanayokumbana nayo ni kama wanyama wakali kama **simba, nyoka, chui, Ghuli, m**ajini na kadhalika. Vile vile kuna **njaa, magonjwa, baridi** na **hali gumu ya maish**a.

Sitiari ya **nyika** inaangaziwa katika beti zifuatazo 435, 733, 968, 1405, 1444, 1485, 1501, na 3682.

Kwa mfano;

Wakiwa kukata **nyika**
wasiwe kupumzika
hata jua likitoka
wakivuta mashauri
(ubt.3682).

Ubeti huu hunaashiria jinsi majeshi yalikuwa yakitembea usiku na mchana kupitia **nyikani** wakienda kupeleleza na pia kupigana. **Nyika** imetumika kama sitiari inayosimamia matezo na matatizo.

Sitiari ya **jabali** pia imetumiwa katika utenzi huu. **Jabali** pia limerejelewa kama **mwamba**, **jiwe** na pia **sakari**, maneno hayo yote yana maanisha kitu kimoja. **Jabali** limetumika kisitiari kusimamia kinga au ngao. Wapiganaji walikuwa mara nyingi wanajikinga na **majabali** au wanatumia **mawe** kuwarushia adui zao. **Majabali** haya pia yalitumiwa kuwapizia adui na kuwapata kwa ghafla bila kutarajia. Mfano mzuri ni kama:

**Jabalini** nikipanda
kule juu nichenenda
na mambo niliyoyatenda
wakitajabu kufari
(ubt. 1418).

Mtunzi anaelezea vile **majabali** yalivyotumiwa katika vita. Isingekuwa ni **majabali** haya, ienda kungekuwa vigumu kushinda vita. **Sitiari ya pango** pia inaashiria mahali pa kujificha kutokana na baridi pia mahali pa kulala usiku na tena kujificha maadui. Haya yanapatikana katika ubeti wa 491.

**Bara, milima** na **bahari** zimetumiwa kama **sitiari ya usuli** ili kuonyesha matatizo waliyokumbana nayo majeshi katika vita. Pamoja na sahaba na viongozi wao. Hii ni ishara ya jinsi mandhari yalivyokuwa upande huo **nyikani**. Beti zinazorejelea mandhari haya ni kama 2691, 3250, 949, 1538, 1862, na 4076 mtawalia.

**Sitiari ya pepo** imetumika kwa namna **tatu** tofauti katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Kwanza kuna kufananishwa mwendo ambao mambo yalikuwa ya kifanywa. Pia kukinga kama **upepo wa kusi** unavyovuma na kwenda kwa mwendo wa kasi bila kuacha nafasi ya kupitia. Sahaba wa Waislamu walijifananisha na upepo wa kusi huvumao kutoka kusini ukiwa na nguvu nyingi na kuvuma kwa mwendo wa kasi. Dhihirisho kamili ni katika ubeti ufuatao:

Akitungia kwa kasi
**yukinga pepo za kusi**
tusikupata nafasi
tusijuana shauri
(ubt.2668).

Mfano huu unaonyesha vile **upepo wa kusi** unavyovuma kwa haraka na nguvu nyingi kiasi cha kwamba hakuna wakati wa kujitayarisha. Beti zingine ni 2009, 2480, 2649, 2669, 1751, 1408, 837, na 3886. Ubeti wa 587 na 676 neno linalotumika ni "kana upepo wa rihi" na "shabibi pepo za rihi". Hata hivyo vyote vinaashiria nguvu na mwendo wa upepo.

Aina ya pili ya sitiari ya upepo ni matumizi ya neno **peponi. Sitiari ya peponi** imetumika kuonyesha mahali pazuri mbinguni ambapo roho za wanja huenda baada ya kufa. Sitiari hii imetumika katika beti zifuatazo 365, 880, 931, 1952, na 4104.

Aina ya tatu ya **sitiari ya upepo** imetumika katika beti zifuatazo 133, 356, 371, na 4181. Zinasema hivi 'wala pepo na nari', "tamdhamini na pepo" "muumba pepo na nari". Aina

hii pia ni sitiari inayorejelea mahali pema **peponi** kwa njia isiyo ya wazi kama kutumia neno peponi ambalo ni kielezi cha mahali.

Sitiari ya **shajari** pia imetumika. Shajari hapa inarejelea **mti** au **miti.** Sitiari hii ni ya kimandhari kuelezea jinsi mazingira yalivyokuwa huko **nyikani.** **Miti** imetumika kama kinga hasa matawi yake kama ubeti huu unavyodhihirisha.

Lianguka intiati
**likinga tawi la mti**
akiyaona mauti
na ajali ashmari
(ubt. 678).

Mtunzi anaelezea jinsi kufari alianguka akijikinga na **tawi la mti** alipoyaona mauti na ajali mbele yake. Sitiari hii ni ya kuonyesha hali ya kutokuwa na kinga kamili. Kwa sababu **tawi la mti** haliwezi kuzuia upanga. Beti zingine ambazo **shajari** imetajwa ni 463, 1499, 1503, 1494, 1498, 1758, 1863, 2816, 1329, 596, 358, 1496, 627, 1800 na 55. Sitiari nyingine ambazo zimetumika ni **nuru, kiza, nyota, mwezi** na **motoni.** Katika sitiari hizi zote kiza ni kinyume.

Vilinganishi hivi vyote vimetumika kujenga sitiari mbali mbali. **Nuru, nyota, jua** na **mwezi** zinaweza kuashiria furaha na amani watakayopata Waislamu baada ya maisha ya dhiki ulimwenguni. Ni sitari za matumaini ya baadaye, zinapatikana katika beti zifuatazo 358, 4370, 1000, 963, 964, 255 na 3682.

Kwa upande mwingine nazo **kiza** na **motoni** ni ishara ya hofu, huzuni, shida, mashaka, ukosefu wa matumaini kwa makafiri. **Kiza** kinaweza kuhusishwa na woga, upweke, msiba, kushindwa, majini na maovu yote yanayojulikana. Ilhali **moto** ni ishara ya huzuni, taaabu, masikitiko, hali ya kutamausha na hatimaye mauti ya milele kwa makafiri.Wa Mutiso (1996). Beti zinazorejelea **kiza** na **moto** ni 255, 299, 477, 586, 631, 1346, 1905, 2443, 4104, 4105 na 4370.

Kuna pia sitiari za vifaa kama vile **sanamu, upanga, chuma, ukuta** na **fimbo.** Sitiari ya **sanamu** ambayo ni **sitiari ya usuli** inatumiwa na makafiri kama Mungu wao. Sanamu hii inasawiriwa kama ndio kinga na nguvu ya makafiri. Kila mara wanaonekana wakiingia mahali imewekwa ili kuabudu. Katika ubeti wa 470, tunaelezwa vile kufari anaingia na kusujudu mbele ya **sanamu** kwa masikitiko makuu. Vile vile katika ubeti wa 473 na 474, tunaelezwa vile ibilisi maluuni anapoondoka na kuingia **sanamuni.** Mtunzi anaendelea kuelezea jinsi **sanamu** inatamka na cheche za moto kutoka. Na moshi kutokea puani kama wingu la mvua.

**Sanamu** inawakilisha kutokuwa na Mungu wa kweli au kutojua kuna Mungu aliye juu ya vyote vilivyoumbwa. Hii ni hali ya kusikitisha kulingana na Waislamu ambao wanaamini Mungu ni mmoja na hana wa kulinganishwa naye. Pia wanaamini Mungu haonekani na hana mfanano.

Kwa upande mwingine Waislamu wanasawiriwa kuwa na Mungu ambaye anawasaidia kushinda katika vita. Beti zinazodhihirisha matumizi ya **sanamu** ni 519, 520, 330, 334, 3278, 1357 na 3533.

Sitiari ya **upanga** pia imetumiwa kuelezea nguvu na uwezo wa kuua adui kwa kutumia **upanga**. Silaha hii imetukuzwa sana katika utenzi huu kwa kuwa iliwawezesha Waislamu kupata ushindi dhidi ya maadui wao.

**Upanga** umetumika kama **sitiari ya usuli** kuashiria vita na mauaji. Ni kwa kutumia **upanga** ambapo ushindi ulipatikana. Beti zifuatazo zinadhihirsha haya 262, 336, 563, 630, 642, 755, 757, 829, 813, 919, 911, 1227, 1254, 1330, 1403, 1437, 1714, 1760, 1826, 1981, 2031, 2139, 2136, 2610, 2752, 2768, 2817, 2888 na 294.

Sitiari ya **chuma** pia imetumiwa kuonyesha kuwa imara, kutotingizika na pia kama kifaa cha vita. Msimulizi anaelezea vile maadui walikuwa wanapigwa kwa **chuma.** Kumaanisha mtu akiwa na **chuma** yuko imara na hana woga. **Chuma** kimetajwa katika beti zifuatazo 1712, 1462, 1434, 1660, 3014, 3021, na 310.

Sitiari nyingine ya usuli iliyotumika ni **sitiari ya fimbo.** Hata hivyo **fimbo** imetumiwa kama kifaa cha kuadhibu wakosaji. Kwa hivyo haikutumika kama sitiari . Kwa mfano.;.

Bali leo utaona
tawakusanya watwana
**wakupige fimbo sana**
na aqili zikuduri
(ubt. 537).

**Fimbo** hapa imetumiwa kama kitubio cha kukanya na kurekebisha. Beti zingine ni kama 1252, 3997 na 4007.

Kwa upande mwingine **fimbo** imetumika kama ishara ya kudhihirisha kuwa mtu fulani alipitia mahali. Mtunzi anaeleza katika ubeti wa 2245. “utwae **fimbo** wa mti na kuusimika njiani ili nione ni kama mti”. **Fimbo** hapa imetumika kama ishara kwamba ni yeye alipitia pale.

Maana nyingine ya matumizi ya **fimbo** inadhihirika katika ubeti wa 2254 na 2255. Hapa ni ishara ya nguvu za Mungu. **Fimbo** inasimikwa chini na kuota matawi saba kwa amri yake Raba.. Kwa hivyo ni sitiari inayoonyesha ukuu wa Mungu..

Kuna aina nyingine za sitiari katika U*tenzi wa Rasi’lGhuli* na sio rahisi kuangazia zote kwa kipindi kifupi kama hiki. Hata hivyo sitiari zile kuu tumeziangazia kwa mapana na marefu.

### 3.1.5 Hitimisho

Katika sura hii ya tatu tumeangazia matumizi mbalimbali ya sitiari katika *Utenzi wa Rasi’lGhuli*. Sitiari zilizotumiwa ni nyingi na zinachangiana katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani. Aina za sitiari ambazo tulichunguza ni sitiari kuu, sitiari sahili, sitiari chakavu, sitiari hisimseto na sitiari za usuli. Hata hivyo aina hizi za sitiari zina ugiligili mwingi na kwa hivyo, sio rahisi kutofautisha baadhi ya sitiari zilizotumika. Sitiari hizi zimejitokeza katika hali tofauti kama vile, sitiari zinazorejelea wanyama, ndege, wadudu, vifaa au vyombo, mahali mahsusi, vitu asilia na hata viumbe dhahania au za kimaajabu.

Matumizi ya sitiari katika Utenzi huu yamesaidia kukuza dhamira na maudhui ya mtunzi, kutambua sifa za wahusika, kuendeleza msuko wa hadithi kwa njia inayovutia na kuonyesha ufundi na ustadi wa hali ya juu wa mtunzi wa kutumia mtindo mwafaka.

Uteuzi wa lugha ili kuleta muumano na muwala umepangwa kwa hali ya juu mno. Ni kupitia kwa matumizi ya sitiari ambapo mbinu nyingi za uandishi zimekuzwa. Kwa mfano tasfida, taswira, chuku, kinaya, jazanda na kadhalika. Tumeweza pia kubaini msimamo wa mtunzi kuhusu makafiri. Mtazamo wa Waislamu kuhusu makafiri. Pia umedhihirika wazi wazi. Hii ni kwa sababu sitiari nyingi zimetumika kudhalilisha makafiri na kutukuza dini ya Waislamu. Maudhui yanayojitokeza kupitia kwa wahusika yanabainisha wazi wazi mtazamo wao kuhusu makafiri.

Hata hivyo, sitiari ambazo zimetumika zimefungamanishwa na utamaduni wa jamii nyingi duniani na kwa hivyo, ni rahisi kueleweka. Mbinu hii imetusaidia sana kudhihirisha kwamba mtunzi amefanikiwa katika kuwasilisha kazi yake kifani.

# SURA YA NNE

## 4.0 Utangulizi

Tumetathmini na kuchambua matumizi ya sitiari, katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani katika sura ya tatu. Tumeona kwamba mbali na kufanikisha kazi kifani, sitiari pia ina uamilifu mwingine ambao ni pamoja na kuwasilisha hisia, mtazamo wa kiitikadi, kutukuza, kudhalilisha na kukweza aina fulani ya dini dhidi ya dini zile zingine. Katika sura hii ya nne tumechunguza matumizi ya tamathali ya takriri katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani.

Kama tulivyosema katika sura ya pili takriri ni mbinu ya kisauti au maneno ya kurudia irabu, konsonanti, silabi au neno katika utungo fulani kwa nia ya kusisitiza na kuweka uthibiti moyoni ili lisisahaulike.

Katika sura hii tutajikita katika kuchunguza matumizi ya takriri irabu/ vokali, takriri konsonanti, takriri neno/maneno, takriri silabi na usambamba. Katika utafiti huu tutatumia dhana ya takriri kama urudiaji unaohusu sauti za lugha. Pia tutachunguza kama ziliweza kuchangia kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani.

## 4.1 Ufafanuzi wa takriri katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani

Takriri ni kipengele mojawapo cha tamathali za usemi. Wamitila (2008). Takriri ni mbinu inayorejelea urudiaji wa sauti, neno au sentensi fulani, pia hujulikana kama uradidi. Kuhenga (1997) takriri ni mtindo wa uneni wa fasaha ambao msemaji kwa makusudi au nia mahsusi hurudia neno au maneno yale yale ili kutia mkazo au msisitizo zaidi juu ya jambo asemalo. Mtindo huu wa maneno wa msisitizo huwa na nia ya kutia nanga jambo fulani ili liweze kumwingia msikilizaji moyoni apate kulithibiti vizuri.

### 4.1.1 Takriri Irabu/Vokali

Sababu za kurudia irabu ile ile katika sehemu sawia za neno katika sentensi ni kuleta wizani au ridhimu katika utungo wa kifasihi hasa katika ushairi. Wamitila (2003) anasema kuna uwezekano ikawa kurudia kunakojitokeza ni matokeo ya sifa za lugha inayohusika tu bali si tendo la kimakusudi la mtunzi fulani.

Katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*, aina hii ya takriri imetumika kwa wingi. Baadhi ya takriri irabu zimetumika mwanzoni mwa mishororo ya beti tofauti. Zingine zimetumika mwishoni mwa mishororo ya baadhi ya beti kama tutakapodhihirisha.

Ili kuthibitisha madai yetu tutanukuu baadhi ya beti kama thibitisho ya ushahidi wetu. Takriri irabu zimetumiwa katika beti nyingi na kwa hivyo tutatoa mifano ya baadhi tu. Kwa kutumia takriri irabu mwanzoni mwa mishororo katika ubeti mmoja, kwa maoni yetu ni njia moja ya mtunzi ya kusaidia kuelewa ujumbe anaotaka kupitisha bila kutumia maneno mengi tofauti ambayo msomaji hangeweza kuyakumbuka. Hii ni kwa sababu *Utenzi wa Rasi'lGhuli* ni mojawapo ya tenzi ambazo ni ndefu zilizowahi kuchapishwa.

Kama si urudiaji huu labda wasomi wengi hawangekuwa na hamu ya kuhusoma. Kwa sababu hungewachosha. Pia ni njia moja ya mtunzi ya kusisitiza ujumbe ili kurahisisha mambo na kuyafanya yasisahaulike. Kuna uwezekano pia wa mtunzi kuwa na upungufu wa maneno na hivyo kulazimika kutafuta maneno yenye silabi zinazofanana ili kuunda maneno yatakayotimiza haja yake. Matumizi ya silabi mwanzoni mwa mishororo si kwa sababu ya kuleta wizani. Huenda ikawa pia ni mbinu ya mtunzi ya kuonyesha umahiri wake katika utunzi wa ushairi.

Katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* mbinu ya takriri irabu imetumika mwanzoni mwa mishororo kadhaa. Kwa mfano:

**A**kipima kwa qiasi
**a**siweze kujilisi
**a**kitoka kwa upesi
nyumbani akidhihiri
(ubt.380).

Silabi **a** imetumika mwanzoni mwa mishororo ya kwanza mitatu. Silabi hii imetumika kama kirejeleshi cha nafsi ya tatu umoja. Hii ina maana kwamba msimulizi alitumia nafsi ya tatu katika kupitisha ujumbe wake. Aina hii ya urudiaji inapunguza matumizi ya maneno mengi na pia kusisitiza mambo haya yote yalitendwa na mtu mmoja. Kupitia kwa njia hii ya urudiaji ujumbe unaeleweka kwa urahisi na pia maudhui yanakuzwa kwa njia ya kuvutia ili kuendeleza muundo wa shairi. Ni njia pia ya kujenga taharuki kwa msomaji ili atake kujua kitakachotendeka baadaye.

Kuna baadhi ya beti ambapo mtunzi alitumia silabi moja katika mishororo yote minne ili kudhihirisha uwezo wake wa kuithibiti lugha.

Kwa mfano,

**A**lii bun Talibu
**a**kangiwa na ghadhabu
**a**kamwegama kilabu
**a**li na ghedhi kathiri
(ubt. 891).

Katika ubeti huu msimulizi ametumia pia nafsi ya tatu kuelezea hali ya mambo ilivyokuwa.  Anasisitiza kwa kutumia silabi **a** mwanzoni mwa kila mshororo ili ujumbe upate kueleweka kwa urahisi kwa kutumia maneno machache.  Aina hii ya urudiaji pia inaweza kuwa ni kwa sababu ya kukosa maneno mwafaka ambayo angetumia ili kuleta maana aliyokusudia.

Kuna beti zingine pia amechanganya matumizi ya silabi na konsonanti katika ubeti mmoja mwanzoni mwa mishororo.  Kwa mfano;

Nyumbani akiwasili
**a**katamka qauli
**a**kita ewe iyali
leo mimi msafiri
(ubt. 381).

Katika mshororo wa kwanza na wa mwisho, mtunzi ametumia konsonanti kuanzia mshororo ilhali katika mshororo wa pili na wa tatu ameanza na irabu **a**.  Mtindo huu wa kuchanganya irabu na konsonanti mwanzoni mwa mshororo, ni njia bora ya kuondoa uzoefu na kuleta hamu zaidi ya kuendelea kusoma.  Usimulizi aliotumia ni mchanganyiko wa nafsi ya tatu na nafsi ya kwanza.  Mwanzoni katika mishororo mitatu ametumia nafsi ya tatu umoja **a** na mshororo wa mwisho akatumia nafsi ya kwanza umoja **mimi.**  Hii ni njia moja ya matumizi bora ya lugha.

Kuna beti nyingi ambazo ametumia mitindo hii ya kuanza na kiambishi **a** kama kirejeleshi cha nafsi ya tatu umoja na pia kuchanganya irabu na konsonanti mwanzoni mwa mishororo ya baadhi ya beti. Mifano ya aina hii inapatikana katika beti kama vile,

273, 385, 386, 393, 404, 415, 416, 667, 674, 698, 719, 810, 891, 896, 903, 910, 913, 1004, 1008, 1089, 1099, 1173, 1205, 1268, 1287, 1290, 1314, 1349, 1388, 1442, 1473, 1486, 1495, 1575, 1580, 1709, 1746, 1810, 1819, 1945, 1970, 2044, 2151, 2365, 2389, 2111, 2510, 2655, 2784, 2921, 3178, 3245, 3276, 3391, 3451, 3630, 3970, 4359, 4457, 4530 na 4583 .

Nimetaja baadhi tu, kwani ni nyingi mno katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Hata hivyo msimulizi aliweza kuonyesha ubingwa wake katika uthibiti wa lugha kwa kutumia nafsi ya pili ambayo haitumiwi kwa wingi na watunzi wengi wa siku hizi. Haya yanathihirika katika ubeti ufuatao:

**U**fikapo huko kwao
**u**tunze sana vikao
**u**jue khabari zao
**u**niletee khabari.
Ubt. 1115).

Katika ubeti huu msimulizi ametumia nafsi ya pili umoja. Ametumia kiambishi **u** kama kiwakilishi cha **wewe**. Msimulizi ametumia nafsi hii ya pili ili kuonya na kusisitiza kwa anayemtuma ili awe mwangalifu. Ni njia pia ya kuondoa uzoefu wa matumizi ya nafsi moja. Kwa maoni yetu ni kwa sababu ya urefu wa utenzi na lugha iliyotumika ya mchanganyiko wa kingozi, kiarabu na Kiswahili. Kwa hivyo kubadilisha nafsi kunasaidia kuleta mvuto na mnato kwa msomaji ili aweze kuendelea kusoma bila kuchoka.

Ili kudhihirisha umahiri wake katika kuthibiti matumzi ya lugha, mtunzi pia amechanganya irabu na konsonanti katika baadhi ya beti mwanzoni. Kwa mfano;

Twaona wajitanabu
huji ukataqarabu
**ukila** ukisharabu
**u**katibu na khatiri
(ubt. 3544).

Katika mishororo ya kwanza miwili mtunzi ametumia konsonanti mwanzoni mwa mishororo.  Nayo mishororo miwili ya mwisho ametumia irabu kuanzia sentensi.  Mtunzi pia amechanganya nafsi.  Katika mshororo wa kwanza ametumia nafsi ya kwanza wingi na nafsi ya pili umoja.  **Twa** ni kirejeleshi cha **sisi** na **wa** cha **wao.**  Mishororo mingine mitatu anaeendeleza nafsi ya pili wewe.

Kwa maoni yetu ni kwamba kwa kutumia nafsi hizi mbili, ni njia moja ya kufanikisha kazi yake kifani. Maudhui yanakuzwa, msuko unavutia, mtindo unapendeza na lugha yote kwa ujumla ni ya kuvutia na kutia moyo wa kuendelea kusoma utenzi bila kukinai au hata kuchoka.

Beti zingine zilizo na mipangilio hii miwili tumeeleza ni 21, 40, 681, 691, 1069, 2901, 4116 na 3544.  Matumizi ya takriri irabu pia yanapatikana kwa wingi mwishoni mwa mishororo ya kwanza mitatu katika beti nyingi sana.  Takriri irabu/vokali zinapotumika mwishoni mwa mishororo, huwa kusudi lake kuu ni kusawazisha vina pamoja na kuleta ridhimu katika beti.

Kwa maoni yetu pia ni kanuni zilizowekwa ili kuzingatiwa katika utunzi wa mashairi ya ya kiarudhi na hasa ya kale.  Hii ni kwa sababu kama si sheria hizi mtunzi angetunga kama shairi huru au vue na bado ujumbe huo uwafikie wasomaji kwa njia bora hata zaidi.

Bora zaidi ni njia ya kupunguza matumizi ya maneno mengi ambayo angetumia katika kuwasilisha ujumbe wake.  Kwa kuwa matumizi ya takriri irabu yametumiwa kwa wingi mwishoni mwa mishororo ya kwanza mitatu, nitatoa mifano michache, halafu nielekeze beti kadhaa ambazo zinaweza kurejelewa.

Kuna baadhi ya beti ambapo mishororo hiyo mitatu inaishia na irabu zenye keketo za aina moja.  Kwa mfano;

Aqili zikawa**paa**
wasihimili kuk**aa**
wakitoka iyo s**aa**
na ndia wakidabiri
(ubt. 4039).

Katika mfano huu msimulizi ametumia matumizi ya irabu **a** mtawalia.  Pia ametumia nafsi ya tatu wingi,  inayowakilishwa na kiambishi **wa** kumaanisha wao.  Ametumia pia vitate paa, kaa, saa kama mbinu ya kupitisha ujumbe.

Kwa kuwa kusudi letu kuu ni kuthibitisha kama mtunzi amefanikiwa kuwasilisha kazi yake kifani, tumechunguza matumizi ya lugha, msuko, mtindo na wahusika na jinsi matumizi ya takriri yameweza kuchangia katika mambo haya.

Kwa maoni yetu lugha anayotumia mtunzi imesaidia kukuza maudhui, kuendeleza dhamira, kutambua sifa za wahusika pamoja na mpangilio mzuri wa msuko wa hadithi na mtindo. Beti zingine zenye mpangilio huu ni 2290, 4098, 4107, 3557, 2580, 2978, 3770 na 4098 .

Hata hivyo kunazo beti zingine zinaishia na **a** lakini zikatanguliwa na **i, e, u** na **o.** kwa mfano;

Kufari wachangali**a**
ya baa kuwashuki**a**
wasiweze vumili**a**
na mbio wakidabiri
(ubt. 2393).

Huu ni mpangilio ambao umetumika kwa wingi kuliko mipangilio ile mingine. Labda ni kwa sababu kuna uwezekano kuwa irabu **i** na **a** zinatumika sana katika kunyambulisha vitenzi vingi kwa kauli ya kutendea. Hata hivyo kwetu ni matumizi ya mnyambuliko wa vitenzi, ambayo ni njia moja ya kuonyesha kufanikiwa kwa mtunzi katika kazi yake kifani.

Beti zingine zilizofuata mpangilio huo ni 495, 528, 538, 601, 607, 618, 651, 717, 724, 728, 784, 845, 857, 900, 916, 957, 965, 989, 1019, 1037, 1064, 1099, 1116, 1121, 1150, 1172, 1240, 1269, 1308, 1313, 1472, 1500, 1575, 1600, 1697, 1785, 1851, 1987, 2163, 2204, 2250, 2760, 2898, 3017, 3340, 3894, 4069, 4257, 4391, 4480 na 4522. Hizi ni baadhi tu ya zilizofuata mpangilio huo wa **a** kutanguliwa na **i**.

Nazo beti ambazo zinaishia na **o** ni kama 340, 1115, 1523, 1619, 1635, 1730, 1779, 1798, 2274, 1313, 2503, 2588, 2940, 2950, 3200, 3260, 3948, 4046 na 4254. Beti hizi si nyingi sana labda kwa sababu sio irabu nyingi zinaweza kushirikiana na kiambishi **o** katika kuunda maneno ya aina hiyo au pengine mtunzi hakupendelea mpangilio huo.

Kwa mfano;

Pasiwe tena kika**o**
wakipenda nyama za**o**
sahaba wachenda na**o**
wasiwe kutaakhari
(ubt. 3948).

Msimulizi ametumia nafsi ya tatu wingi katika kupitisha ujumbe. Huu ni utumiaji wa lugha kiufundi ili kusisitiza kwa kurejelea watenda. Pia kuna beti zingine ambazo msimulizi ametumia irabu **e** kama kiishio.

Na weye sinikhofi**e**
na wataka waniji**e**
nawe hapa wangali**e**
nitakavyo wadamiri
(Ubt. 600).

Mpangilio huu sio mwingi katika utenzi huu. Labda pia kiambishi **e** hakina ushirika wa karibu na irabu zingine kwa wingi. Hata hivyo kwa upande wetu ni njia bora ya kudhihirisha ufundi wa mtunzi wa kupitisha ujumbe kwa kutumia aina nyingi za irabu na

kuondoa mazoea ya kutumia aina fulani za irabu. Labda pia alikuwa akitaka kushirikisha irabu za kigeni katika kazi yake ili kuikuza lugha ya kiarabu ambayo irabu nyingi zinatokana na hati za kiaribu.

Kwa ujumla kuna beti nyingi ambazo zimetumiwa mwishoni mwa mishororo mitatu ya kwanza katika utenzi huu. Kwa mfano; 68, 87, 89, 109, 413, 414, 532, 620, 830, 1037, 1152, 1127, 1294, 1483, 1523, 1796, 1933, 2274, 2314, 3310, 3528, 3666, 3952, 4097, 4170, 4348 na 4549.  Hizi ni baadhi tu, kuna beti nyingi ambazo zimeishia na irabu tofauti tofauti.  Mpangilio huu umewezesha mtunzi kuyakuza maudhui yake zaidi na pia kusaidia kuwaelewa wahusika wake na sifa zao pamoja na kuonyesha uelewa wake wa kuoanisha mofu, virai, vishazi na sentensi ili kuleta athari kwa kazi yake, na pia kwa msomaji. Matumizi haya mazuri ya lugha yanachangia pakubwa katika ufanisi wa kazi yake kifani.

Nikimalizia sitasahau kunukuu baadhi ya beti ambazo mtunzi amebadilisha mpangilio wake wa kumalizia mishororo ya tatu ya kwanza katika beti na labda irabu au konsonanti.

Kuna beti ambazo mtunzi amechanganya irabu na konsonanti katika ubeti mmoja kama kiishio. Kwa mfano;

Wachenenda sawa saw**a**
wasiwe na kupumu**a**
hata alipouaw**a**
babaye akibusuri
(ubt.1383).

Hapa msimulizi amechanganya irabu na konsonanti. Labda ni mbinu yake ya kuondoa uzoefu au pia kuonyesha utaaalamu alio nao wa lugha. Pia aliweza kuwa amekosa neno mwafaka ya kujaza sehemu hiyo ili ujumbe ukamilike. Beti zingine za aina hiyo ni 1602, 2134, 2277, 2671, 2755, 2891, 2903, 3110, 3112, 3114, 3166, 3277, 3744, 3784, 3785, 4054, 4276 na 4349.

Kwa kutumia takriri irabu mtunzi aliweza kudhihirisha ubunifu wa hali ya juu katika mpangilio, uteuzi, uchanguzi na utumiaji wa maneno kwa ufasaha. Maudhui yaliweza kukuzwa na kuendelezwa. Sifa za wahusika zimedhihirika, msuko ukasukwa ukasukika na mwishowe ujuzi wa kutumia nafsi zote katika usimulizi ukabainika.

### 4.1.2 Takriri Konsonanti

Aina hii ya takriri hujitokeza wazi katika kazi ya ushairi. Wamitila (2003) anaeleza kuwa istilahi hii hutumiwa kuelezea urudiaji wa sauti ya konsonanti. Kimsingi kurudia huku hutokea mwanzoni lakini kuna uwezekano wa kupatikana pengineko.

Licha ya kuchunguza mahali zimetumika na jinsi zimetumika konsonanti hizi, mwegemeo wetu ni kama zimesaidia kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani.

Katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* takriri konsonanti zimetumika. Baadhi zimetumika kama njia ya kusisitiza ujumbe. Kuna zile zimetumika kukamilisha sentensi ili kuleta usawa wa mizani katika ubeti. Kuna takriri konsonanti zingine ambazo zimekuwa mshororo mzima labda kudhihirisha ukwasi wa mtunzi katika matumizi ya lugha.

Aina hii ya sitiari haikutumika kwa wingi katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Hata hivyo, hiyo sio muhimu sana kwetu kwa sababu tunaitaji mifano michache tu, ili kudhihirisha,

kwamba mtunzi amefanikiwa katika kazi yake kifani. Baadhi ya takriri konsonanti ambazo zimetumiwa kwa namna ya kusisitiza ni kama neno **himahima.**

Kwa mfano;

Niletee **himahima**
sefu yangu samsama
ndiyo siku ya heshima
ya kwondoa leo ari
(ubt. 2763).

Matumizi ya takriri **himahima** ni kama kusisitiza yaani moja kwa moja au haraka haraka. Kule kutumika mwishoni mwa sentensi ni njia ya kusawazisha mizani katika ubeti na vile vile kuonyesha ujuzi katika matumizi ya lugha. Hata hivyo ni mfano mzuri wa kubadilisha mpangilio wa virai hili kuondoa mazoea.

Katika beti zote ambazo takriri hii imetumika, imeleta dhana moja ya kusisitiza ingawa imetumika na maneno mengine kama **anakuja himahima, achondoka, achenenda, akitoka**, na **wanakuja himahima**. Mfano wa beti hizo ni 502, 909, 971, 1354, 1382, 1398, 1540, 2478 na 2624.

Mfano mwingine wa takriri konsonanti ni neno **kalikali.** Takriri hii imetumika pia mwishoni mwa mshororo kwa nia ya kusisitiza na pia kusawazisha vina. Beti zote ambazo neno hili limetumika liliambatanishwa na neno dharuba isipokuwa ubeti wa 2494 ambapo limetumiwa kuonyesha sauti **kalikali.** Msisitizo wa aina hii unasaidia kuwaelewa wahusika na tabia zao. Pia ni njia mwafaka ya kukuza dhamira ya mtunzi

pamoja na kuendeleza msuko na muundo wa hadithi. Beti zilizoandikwa takriri **kalikali** ni 806, 898, 1651, 1661, 2035, 2881, 2746, na 4526. Mfano wa jinsi neno hilo lilivyotumika ni kama katika ubeti huu;

Akishitadi juhali
kwa dharuba **kalikali**
kuua saba rijali
wote akiwakhasiri
(ubt. 2035).

Ni mfano wa majisifu kwa waislamu jinsi walivyokuwa wakiwaua makafiri. Takriri nyingine ambayo imetumiwa sana na makafiri kama kiapo ni neno **naapa uza na lata** na mara nyingine **naapa lata wa uza**. Hii ni njia ya kusisitiza kwa uwezo wa Mungu wao. Kumaanisha hakuna kurudi nyuma katika jambo analotaka kufanya. Ni sawa na kusisitiza uwezo wa huyo Mungu wao. Takriri hii imetumika kama mshororo mzima labda kuonyesha umuhimu wa kiapo hicho. Mfano wa matumizi ya takriri hii ni kama ufuatao:

**Naapa lata wa uza**
tamuonya miujiza
ajaliye imesoza
wakisha wake umuri
(ubt. 2622).

Beti zenye matumizi ya takriri hii ni 285, 1053, 1054, 1195, 1241, 1610, 1670, 1622, 3631, 2622 na 1062. Takriri nyingine ambayo imetumika ni ya kiarabu. Imetumika kama

njia ya kusisitiza na kuonya Waislamu na pia kama njia ya kuthibitisha ukweli wa mambo. Kwa mfano;

**Qala rawi 'lkalamu**

khabari za islamu

tuziweke maalamu

turejee kwa kufari

(ubt. 1897).

Takriri konsonanti hii imetumika kama mshororo mzima labda kwa njia ya kubadilisha msimbo. Yawezekana pia ni njia ya kuitambua lugha ya Kiarabu. Hii ni kwa sababu asili ya hadithi hii ilikuwa ya Kiarabu. Pia inawezekana mtunzi hakutaka kupoteza maana asili ya ujumbe alioutaka kuwasilisha. Kwa sababu maneno mengine yakitafsiriwa yanakosa maana halisi au kupunguza uzito wa maana hiyo.

Hata hivyo,kwetu pia ni mbinu ya kifasihi ya kuhamisha ndimi au kubadilisha msimbo. Maneno mengine sawa na haya ni **Qala rawi ikhabari** beti, 1903, 3428, na 4201. **Qala rawi'lkalamu,** 544, 592, 1343, 1897, na 4330. **Qala rawi 'lkitabu**,1524, na 4470. **Qala rawi 'lkalama,** 709, 3186 na 3890. **Qala rawi msanifu,** 1988. **Qala rawi tabain** 567.

Kuna takriri konsonanti za aina tofauti kimaneno ambazo zimetumika lakini kwa nia moja ya kusisitiza. Tutazitaja tu, ili kuthibitisha uwepo wa aina hizi za konsonanti. Kuelezea zaidi ni sawa na kurudiarudia yale tumekwisha elezea. Hata hivyo, ni thibitisho kwetu mtunzi amefanikisha kazi yake kifani. Takriri hizi ni kama zifuatazo. **Mmoya mmoya** beti 4225, 4382, na 4389. **Mivumbivumbi** beti 2576, 3356, 3933. **Babubabu** 1524, 1578. **Sawasawa** 1383, 2424. **Tungutungu** 457, **Haihatihaihati** 2749, **palepale**

1902, 1929, **kisukasuka** 1908, **njemanjema** 2781, **mbalimbali** 2248. **Polepole** 1069. **Tamutamu** 1200. **Memamema** 1103. **Dhaifu dhaifu** 3510 na kadhalika.

Matumizi ya takriri konsonanti ni mojawapo ya mbinu za kifasihi na mtunzi amezitumia kwa njia ya hali ya juu sana. Mara mwanzoni mwa mshororo, katikati, mwishoni na tena kama mshororo mzima. Huu ni ubunifu wa hali ya juu sana.

### 4.1.3 Takriri Neno/Maneno

Aina hii ya takriri hutumiwa kuelezea urudiaji wa maneno au neno fulani katika matini au kazi fulani. Hii ni njia mojawapo ya kusisitiza jambo au hata kuchezea maneno ya utungo wenye takriri.

Aina hii ya maneno imetumika kwa wingi katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Baadhi ya maneno yamejitokeza kwa wingi sana. Kwa mfano, neno **baada** limesheheni karibu kila ukurasa. Neno hili limetumika kuelezea matukio yaliyopita yaani kama mbinu rejeshi au kisengere nyuma. Pia neno hili wakati mwingine limetumiwa kama **baadaye.**

Kwa maoni yetu ni kwamba, kwa sababu mtunzi ametumia nafsi ya tatu kwa wingi, hakuwa na budi kulitumia neno hili ili kuunganisha matukio yaliopita. Pia kwa sababu ni hadithi ambayo ilikuwa ikisimuliwa tangu zamani hakuwa na budi kutumia neno **baada** au **baadaye** katika tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili.

Kwetu sisi pia ni mojawapo ya mbinu ya uandishi ambayo inaipa kazi ya mtunzi sura na mnato kwa wasomaji. Ni njia ya kurahisisha maelezo kwa kupunguza matumizi ya maneno mengi ambayo yangechosha. Hasa ikizingatiwa urefu wa utenzi huu.

Hapa tutanukuu ubeti ambao takriri hii imetumika kama mbinu rejeshi halafu tutataja baadhi ya beti kama marejeleo kwa sababu ni nyingi sana.

**Baada** ya kukeleti
nikasikia sauti
ikasukasuka inti
majabali na shajari
(ubt.463.)

Mtunzi anaelezea kwa kutumia nafsi ya kwanza jinsi alivyosikia sauti ambayo ilitingisha nchi, miamba na miti. Hapa neno hili linatumika kama kirejeshi cha wakati uliopita badala ya kusisitiza.

Kwa upande mwingine neno hili pia limetumika kuonyesha mambo yale yaliyofuatia baada ya kitendo fulani. Hii ndio sababu neno hili linabadilishwa umbo na kutumika kama **baadaye**. Kwa mfano;

Hiepuka ile ndia
kwenda msita ngamia
**baadaye** harejea
na ndia haidabiri
(ubt.447).

Matumizi ya neno hili hapa yamebadilika. Ni tofauti na hapo mwanzo. Hapa anaelezea yalioyofuatia baada ya kuepuka njia aliyoambiwa asipitie.

Sababu hizi na zile tulizotangulia kusema ndizo zinaifanya neno hili kutumiwa kwa wingi. Baadhi ya beti ambazo maneno haya yalitumiwa ni 302, 429, 557, 625, 731, 1029, 1128, 1275, 1300, 1397, 1429, 1426, 1517, 1596, 1611, 1628, 1781, 1809, 2032, 2126, 2167, 2221, 2252, 2267, 2305, 2370, 2400, 2444, 2501, 2516, 2542, 2682, 2665, 2788, 2830, 2917, 3000, 3054, 3165, 3229, 3313, 3370, 4372 na 4522. Kuzitaja beti zote ni sawa na kutaja utenzi wote kwa sababu takriri hii imesheheni kote katika utenzi. Kwa hivyo tumechagua mifano hii bila kufuata mpangilio wowote.

Aina nyingine ya takriri neno ambayo imetumika kwa wingi ni **wachenenda** ambayo pia imetumika katika maumbo tofauti lakini maana ni moja. Maneno haya ni **chenenda, enenda**, **takwenda, achenda nichenda, chenda lichenda**. Ni kama kunyambulisha neno hili kulingana na mukhtadha wa wingi na umoja.

Sababu ya kutumika sana ni kusisitiza jinsi kila wakati watu walikuwa mbioni kupigana, kurudi kutoka kwa mapigano, kwenda kupeleleza yaani kila mara walikuwa safarini. Msimulizi hakuwa na budi kutumia neno hili, ili kuelezea hali ya mambo. Uteuzi wa neno hili la kingozi ulikuwa wa kusisitiza kwamba watu hawa hawakuwa wanatulia. Kila wakati ni vita. Ni mbinu ya lugha kifasihi kwa hivyo, tutaichukulia katika mukhtadha huo. Kwa hivyo ni mbinu ya mtunzi ya kuteua maneno kwa njia ya ufundi ili kuwasilisha ujumbe wake kwa njia inayofaa. Takriri hii pia imetumika katika beti nyingi. Tutatoa mfano mmoja na kuorodhesha baadhi ya beti hizo bila kufuata utaratibu wowote.

Muhayii akitoka
**achenenda** kwa haraka
baada alipofika
maneno akiqariri
(ubt. 219).

Takriri hii imetumika mwanzoni mwa mshororo, katikati na hata mwisho. Kupitia kwa matumizi bora ya neno hili, mtunzi ameweza kuangazia mambo mengi ya muhimu. Yakiwemo jinsi vita vilivyopiganwa, watu walivyouawa, wengine kutoroka, wengine kusilimu, kushindwa na kushinda na kadhalika. Msuko wa hadithi pia uliendelezwa na matumizi ya takriri hii pamoja na sifa za wahusika.

Baadhi ya beti zilizoandikwa maneno haya ni 221, 256, 1316, 1331, 1383, 1418, 1460, 1469, 1473, 1494, 1495, 1504, 1645, 1783, 1892, 1960, 2045, 2164, 2174, 2812, 2922, 3000, 3202, 3228, 3598, 36660, 3702, 3770, 3815, 3913, 3995, 4061, 4125, 4172, 4327 na 4366.

Takriri neno ambalo pia limetumika kwa wingi ni neno **khabari.** Neno hili lina maanisha habari na ni la asili ya kiarabu. Kwa maoni yetu neno hili limeteuliwa kwa sababu katika mazingira ya vita habari ni muhimu sana. Kila wakati wapelelezi walikuwa mbioni kwenda kupeleleza habari za adui wao. Mahali walipo, mipango yao, nguvu zao, viongozi wao na uwezo wao. Kwa hivyo, neno **khabari** hapa linasisitiza umuhimu wa kujua ziadi juu ya adui. Neno hili limetumiwa na pande zote mbili. Hata hivyo, limetumika kisanii ili kuchangia katika muundo na mtindo wa utenzi huu.

Kwa mfano;

Mle katika kalama
ghulamu akitazama
umari anvyosema
kwelezea zake **khabari**
(ubt. 1137).

Beti zingine ni 1139, 1167, 1173, 1270, 1281, 580, 588, 604, 710, 926, 1021, 1069, 1075, 1115, 1331, 1349, 1374, 1504, 1524, 1552, 1737, 2191, 2209, 2329, 2395, 2426, 2590, 2635, 2838, 3112, 3116, 3260, 3261 na 3291.

Takriri neno nyingine inayokaribiana na hiyo ni **Tumwa.** Huyu ndiye mara nyingi kwa upande wa Waislamu alikuwa akirejelewa kama Mtume Muhamadi. Neno hili lilirejea Mtume wa Mungu ambaye anaheshimiwa sana na Waislamu. Matumizi yake pia ni ya kusisitiza umuhimu wa Mtume Muhamadi katika dini ya Waislamu. Mfano katika utenzi juu ya matumizi ya takriri hii ni;

Alii akamjibu
akamwambia qaribu
nikuonyeshe habibu
**Tumwa** wa mola Jabari
(ubt. 62).

Mfano huu unadhihirisha kuwa neno hili linarejelea mtu mmoja. Kwa sababu ukitazama beti zingine, ni Mtume Muhamadi anayerejelewa kama Tumwa. Beti hizi ni 63,69,124, 78, 1974, 1997, 2003, 2043, 2056, 2133, 2162, 2209, 2285, 2300, 2319, 2417, 2418, 2524, 2603, 2700, 2808, 2895, 2975, 3010, 3068, 3083, 3347, 3422, 3572, 3879, 3903, 4016, 4042, 4153 na 4234. **Kufari, nyika, kilabu, simba, jabari** ambazo nilielezea kwa

kina katika sehemu ya sitiari ni takriri. Ieleweke hapa kwamba kuna mwingiliano wa matumizi haya ya maneno ingawa maana ni tofauti.

Maneno mengine ambayo yametumika sana na sikuyaelezea awali ni **utamboni** yaani mahali pa vita. Matumizi yake ni sawa na takriri zile zingine kwa sababu yanasisitiza juu ya vita. Beti zilizorejelea neno hili ni 645, 652, 817, 843, 846, 850, 896, 910, 1583, 1680, 1762, 1804, 2010, 2068, 2127, 2435, 2640, 2710, 2827, 2946, 3003, 3015, 3377, 3411, 3638 na 4073. Neno **inti** kumaanisha nchi pia limetumika kwa madhumuni yale yale ya kuelezea mahali walipokuwa wakipigania. Beti nyingi zimerejelea neno hili nazo ni 302, 311, 323, 532, 555, 610, 722, 1145, 1175, 1506, 1594, 1621, 1747, 1862, 1970, 2094, 2275, 2849, 2987, 3620, 4125 na 4380.

Takriri nyingine sawa na hizo zingine kimatumizi ni **iyo ini** kumaanisha wakati huo huo, au sasa hivi. Inasisitiza muda wa kufanya jambo kwa wakati uliohitajika. Beti zifuatazo zimerejelea neno hilo 1300, 1399, 1421, 1896, 1964, 2046, 2126, 2397, 2443, 2556, 2604, 2638, 3064, 3185, 3273, 3593, 3611, 3765 na 3767..

Takriri **khatari** pia imetumika kwa wingi kusisitiza juu ya hatari zilizokuwepo huko **nyikani** na mandhari ya vita. Beti zilizorejelea takriri ya **khatari** ni 594, 625, 651, 835, 1006, 1058, 1189, 1314, 1508, 1796, 1843, 1952, 1999, 2017, 2194, 2202, 2466, 2541, 2804, 2900, 3152, 3992, 4023, 4289 na 4577 .

Kuna aina nyingi za takriri neno ambazo zimetumika lakini zile zimetumika kwa wingi tumezirejelea kwa kina. Nia yetu hasa si kutambua kila aina ya sitiari au takriri iliyotumika bali ni kutafuta ithibati kwamba kwa kutumia mbinu hizi za tamathali, mtunzi aliweza kufanikisha kazi yake kifani.

### 4.1.4 Takriri Silabi

Takriri silabi ndiyo aina ya urudiaji ambayo inapatikana kwa wingi katika tungo za kishairi. Silabi zinazorudiwa mara nyingi huwa muungano wa konsonanti na vokali. Ingawa mara nyingi takriri silabi hupatikana mwishoni mwa mishororo, kuna zile zinazojitokeza mwanzoni mwa mishororo. Katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* aina zote mbili zimejitokeza waziwazi. Zikitokea mwanzoni mwa mshororo huwa ni njia moja ya kusisitiza neno husika. Pia huwa ni ujuzi wa mtunzi wa kuchezea maneno. Inaweza kuwa pia ni mbinu ya kubadilisha mpangilio wa maneno ili kuvunja mazoea. Yawezekana pia kuwa ni mtindo wa kupunguza maneno yatakayotumiwa hasa katika tungo ndefu kama huu wa Rasi'lGhuli.

Tumeangazia baadhi ya takriri silabi zilizotumiwa na mtunzi mwanzoni mwa mishororo na kisha kurejelea zile zilizotumiwa mwishoni mwa mishororo. Baadhi ya takriri za mwanzoni mwa mishororo ni:

**Wa**kithuru shujaani
**wa**ume wapige kani
**wa**kiwandana ndiani
**wa**siwapate khabari
(ubt.1075).

Katika ubeti huu mtunzi ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu ili kuelezea jinsi walivyofanya warejelewa. Msisitizo huu unawarejelea watenda. Kuna baadhi ya beti pia zinachanganya mpangilio huu kwa kuanza na takriri silabi katika mishororo ya kwanza

mitatu halafu mshororo wa mwisho unakuwa kinyume. Hii ni mbinu ya mtunzi ya kuteua mpangilio atakaofuata ili kuvunja uzoefu. Kwa mfano:

**Wa**tatokea rijali
**wa**tu mia abutali
**wa**metukua jamali
pamwe na mayi kathiri
(ubt.982).

Hata hivyo ni vizuri kukiri hapa kwamba mtunzi ametumia ufundi wa hali ya juu katika kutumia silabi za mwanzo. Hii ni kwa sababu mara anatumia mishororo miwili ya kwanza kuchukua silabi zenye keketo za aina moja. Mara nyingine anatumia mishororo miwili ya mwisho. Na tena pia anatumia mishororo miwili ya kati. Huu ni ujuzi unaohitaji utaalamu mwingi. Beti zifuatazo zina mipangilio hiyo yote nimetaja. 438, 493, 549, 560, 563, 731, 732, 744, 982, 1075, 1084, 1339, 1340, 1359, 1490, 1491, 1519, 1522, 1535, 1558, 1692, 1712, 1783, 1789, 1792, 1799, 1831, 1856, 1875, 1895, 2141, 3230, 3765, 3858, 3909, 4350, 4359, 4448 na 4544.

Takriri silabi nyingine ambayo pia imetumika kwa wingi ni '**na**' kwa mfano:

Uwe katika neema
**na** abidi ukituma
**na** zakula zemazema
**na** libasi ya hariri
(ubt.1185).

Mtunzi pia ametumia mpangilio ule wa kubadilisha takriri kuwa mwanzo, katikati au mwisho katika mishororo yote minne. Hii ina maana kuwa mishororo ya kwanza miwili inaweza kuanza na takriri ‘**na’** katika ubeti mmoja na ubeti mwingine mshororo wa pili na watatu kufanana na wakati mwingine mishororo miwili ya mwisho kuanza na silabi zinazofanana.

Aina nyingine za takriri silabi zilizotumiwa mwanzoni mwa mishororo ingawa kwa uchache ni;

**‘hi’** 495, 1420,

**‘ya’** 640, 1286, 1718, 3310

**‘ka’** 707, 896, 1013, 1268

**‘tu’** 1029, 1030, 1568, 1569

**‘la’** 1327 na **‘ndi’** 2128 .

Matumizi ya takriri silabi mwishoni mwa mshororo katika ubeti ni jambo la kawaida katika mashairi ya kiarudhi. Kusudi lake kuu huwa ni kuleta ridhimu na kusawazisha vina katika ubeti.

Katika *Utenzi wa Rasi’lGhuli* mpangilio huu upo ingawa kwa ufundi wa hali ya juu. Uteuzi wa maneno na silabi ni wa kuvutia sana. Mtunzi ametumia aina nyingi za silabi mwishoni mwa beti. Na hasa mishororo ya kwanza mitatu.

Baadhi ya silabi zilizotumiwa mwishoni mwa mishororo mitatu ya kwanza ni **hi, mi, li, ni, bu, di, ngu, fu, si, mu, ni, sa, ma, ya, ka, ti, qu, we, me, ki, ke, qa, ra, tu, za , ta, vu, nde, ko, nga, nda, yo, zi na bi**. Silabi hizi sio za kutafuta zimesheheni katika Utenzi wote na zinatumika karibu kila ukurasa.

Hata hivyo kuna silabi katika maneno ya **kiarabu, kingozi** na **Kiswahili** na zote zimetumika japo kwa beti tofauti na kuchangiana pamoja ili kukuza dhamira na maudhui ya mtunzi pamoja na msuko na mtindo kwa ujumla. Mfano wa silabi katika maneno ya kiarabu zilizotumiwa ni kama;

Hujui mola khali**qi**
maruzuqu mahalu**qi**
ghariba na mashari**qi**
walo bara na bahari
(ubt.521).

Lahaja ya kingozi pia imemtumika sana katika utenzi huu. Labda ni kwa sababu maneno mengi ya wakati huo yalikuwa ya kingozi. Ama mtunzi anatoka maeneo hayo ambayo kingozi hutumika kwa wingi. Lakini kwa maoni yetu hii ni mbinu ya mtunzi ya kuchanganya ndimi na kuhamisha msimbo ili kuleta mvuto na mnato katika kazi yake. Mfano wa silabi katika maneno ya kingozi ni kama ufuatao;

Baada ya kukele**ti**
akiwamo kula quti
sisaze hata kati**ti**
mikate wala hamri
(ubt. 781).

Kuna beti nyingi zinazotumia silabi za maneno ya **kingozi,** mfano, zinazoishia na silabi **di, nga, ma** na kadhalika

Silabi za maneno ya **Kiswahili** ni nyingi pia katika utenzi huu na sina budi kunukuu angalau ubeti mmoja.

Baada hayo kupa**ta**
na mengine atafu**ta**
ya sisi kumfua**ta**
hayo muhali kujiri
(ubt.1604).

Aina hii ya takriri huwa inaeleweka kwa urahisi. Hata hivyo matumizi ya lugha ndiyo hutofautisha mtunzi na mwingine. Kwa mfano, mtunzi wa utenzi huu ameteua silabi za aina nyingi ambazo alizitumia katika kazi yake. Ni watunzi wachache ambao wanaweza kutunga utenzi mrefu kama huu na kuufanya uweze kuvutia wasomi wengi.

Kuna aina nyingine ya takriri ambayo pia mtunzi ametumia. Takriri hii ni **usambamba.** Hii ni aina ya urudiaji ambapo maneno, virai, vishazi au hata sentensi zinawekwa pamoja katika mpangilio maalumu.

Robinson (1970:260) anasema kwamba wakati mpangilio wa maana ya neno unapotumiwa kwa wingi au kuongezewa kwa njia ya kuunganisha sehemu kadhaa kwa ujumla wa mpangilio uliosawazishwa, unaitwa **usambamba.** Mfano wa aina hii ni matumizi ya takriri **ndimi** kwa wingi, hasa wakati viongozi wanapojitambulisha kwa maadui wao kwa njia ya kujigamba. Kwa mfano;

Kisema ndimi sayidi
**ndimi** thabiti fuadi
**ndimi** mvunda junudi
**ndimi** shujaa jasuri
(ubt.1598).

Usambamba mwingine kama huu unapatikana katika beti zifuatazo, 1582, 1805, 2010, 2466, 2738, 2818, 2819, 3368, 4268, 4269, 4270 na 4495. Takriri nyingine ya usambamba sawa na hiyo ni matumizi ya **ndiwe.** Kwa mfano:

.**Ndiw**e sayidi karimu
**ndiwe** shujaa adhimu
kwa arabu na ajamu
**ndiwe** batali jasuri
(ubt.2016).

Beti zingine ni 149, 4281 na kadhalika. Pia neno **wala** katika ubeti wa 356 na 358. Matumizi ya **usambamba** ni ya kusisitiza umaarufu wa shujaa, labda akijisifu au akisifiwa na wengine. Mpangilio huu unahitaji utaalamu mwingi.

Kuna mifano nyingi katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* ambayo hatukuangazia. Hii ni kwa sababu ithibati tuliokuwa tunataka tayari tumepata na tumeweza kuthibitisha madai yetu kikamilifu.

### 4.1.5 Hitimisho

Tumechunguza kwa mapana na marefu matumizi ya takriri katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* na jinsi zilivyochangia katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani. Aina za takriri ambazo tulichunguza ni **takriri irabu/vokali, takriri konsonanti, takriri neno/maneno**, **takriri silabi** na **usambamba.**

Tumebainisha kuwa, mtunzi alikuwa bingwa wa kuteua maneno, virai vishazi na hata sentensi. Aina za takriri alizotumia zilichangia pakubwa katika kufikia lengo lake. Uteuzi huu wa irabu, konsonanti, silabi na maneno ulimwezesha kuendeleza msuko wa hadithi katika mpangilio wa kuvutia na kupendeza.

Aidha kupitia kwa matumizi mazuri ya tamathali hizi za usemi, aliweza kuibua dhana zingine. Hizi ni kama sifa za wahusika, muundo wenye mpangilio unaofuata sheria za utunzi wa mashairi ya kiarudhi, tamathali zingine za usemi kama tasfida, taswira, chuku, jazanda, tashbihi na kadhalika.

Mtunzi pia alitumia weledi wake katika mpangilio wake. Alihakikisha kwamba maneno yametumika vizuri kwa kubadilisha silabi na vina karibu katika kila ubeti. Baadhi zilitumika mwanzoni mwa mishororo na zingine mwishoni mwa mishororo.

Mpangilio huu ulisaidia pakubwa kwa kuwatia moyo wasomaji kuendelea kusoma bila kukinai. Matumizi mazuri ya taharuki yamechangia kuwatia moyo wasomaji, ili kujua kilichotokea baadaye. Msisitizo wa baadhi ya maneno pia umesaidia kurahisisha kazi kwa msomaji. Kwani ni njia moja ya kupunguza idadi ya maneno. Kwa ujumla mtunzi amefanikisha kazi yake kifani. Kwa sababu vipengele vyote vya fani vimetumika na kuchangiana katika kuendeleza msuko wa hadithi. Matumizi ya mbinu ya kubadilisha

msimbo pia yalisaidia sana kuondoa uzoefu wa aina nyingi za mashairi na hasa ya kisasa ambapo lugha ya Kiswahili ndiyo tu hutumiwa.   Kupitia kwa matumizi mazuri ya takriri na sitiari mtunzi aliweza kuwasilisha ujumbe aliokusudia kwa njia mwafaka.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumerejelea muhtasari wa yale tumeyashughulikia na kuyaangazia katika utafiti wetu. Tumetathmini malengo ya utafiti wetu pamoja na kupima nadharia tete za utafiti huu. Kando na hayo, pia tumetoa mwelekeo na mapendekezo ya tafiti za baadaye. Uhakiki wetu umechunguza jinsi takriri na sitiari zimetumika ili kufanikisha kazi ya mtunzi kifani katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*.

## 5.1 Malengo ya utafiti wetu

Lengo la kwanza katika kazi yetu lilikuwa limelenga kutumia uhakiki wa kimuundo kufafanua takriri na sitiari katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Tumefanikiwa vilivyo kwani tuliweza kutambua na kuangazia jinsi takriri na sitiari zilivyotumiwa na mtunzi kwa wingi na jinsi mbinu hizi zilivyochangia kufanikikisha muundo wa utenzi wote kwa jumla. Kama si matumizi mazuri ya mbinu hizi mbili, bila shaka utenzi huu labda haungekamilika na kutambuliwa kama mojawapo ya tenzi za kale.maarufu..

Aidha matumizi ya takriri na sitiari yamefanikisha kazi ya mtunzi kifani, kwani muundo wake ambao ulichangiwa pakubwa na mbinu hizi mbili, uliweza kusaidia kuziteka fikra za msomaji kwa njia ya urahisi. Pia muundo wa kurudiarudia baadhi ya silabi na maneno katika utenzi wote, kulichangia kupunguza idadi ya maneno na kuhufanya ueleweke kwa urahisi. Hata hivyo tuliweza kuelezea haya yote kwa mapana na marefu katika sura ya pili, tatu na ya nne.

Lengo letu la pili, lilikuwa ni kubainisha jinsi tamathali hizi mbili zilivyofanikisha kazi ya mtunzi kifani. Kwa kweli lengo hili ndilo lilikuwa uti wa mgongo katika utafiti wetu. Katika sura ya tatu na ya nne tuliweza kuibua dhana tofauti ambazo zilichangia pakubwa katika kufanikisha kazi ya mtunzi wa utenzi huu. Kwanza kabisa, ni vizuri ieleweke kwamba fani ni vipengele vya kisanii vitumiwavyo kuyawasilisha maudhui. Fani pia huwa na uamilifu wa kuupa utungo wa kifasihi umbo mahsusi. Umbo lenyewe linaweza kuwa la ndani au nje. Katika tungo za kishairi, umbo la ndani hujengwa kwa vipengele vya fani kama vile matumizi ya lugha, wahusika, mandhari, msuko, usimulizi, toni na kadhalika. Nalo umbo la nje hujengwa kwa vipengele vya fani kama vile beti, mishororo, mizani na vina .

Masuala haya yote yanachangiana na kujengana na sio rahisi kuyatenganisha. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* matumizi ya takriri na sitiari yaliweza kusaidia katika kuendeleza vipengele hivi vyote kama tulivyoangazia katika sura ya tatu na ya nne.

Kupitia kwa mbinu hizi mbili tuliweza kutambua msuko wa hadithi, sifa za wahusika, muundo wa utenzi wote, mtindo wa kazi ya mtunzi, aina za simulizi alizotumia, mandhari, lugha, toni na kadhalika.

Bila shaka, hii ndio sababu wataalamu wa nadharia ya umuundo wanasisitiza na kutilia mkazo uhakiki wa kifani, katika kufasiria matini na kupima kufana au kufeli kwa mtunzi katika kazi yake ya usanii.

Lengo letu la tatu lilikuwa kueleza na kufafanua dhana za takriri na sitiari pamoja na aina za kila mojawapo na kisha kuzichambua.  Katika sura ya pili tulishughulikia lengo hili kwa kina.  Kwa kurejelea maoni ya  baadhi ya wataalamu mbalimbali waliozungumzia zaidi juu ya dhana hizi mbili.  Wataalamu hawa ni kama vile Abrahams. M.H. (1974) *Glossary of Literary Terms*: *Toleo la tatu*, New York: Holt, Reinehart and Winston Inc, Scott A.F. (1983) *Current Literary Terms*: A Concise Dictionary, London, Macmillan, Habwe J. (1999) ‘*Discourse: Analysis of Swahili Political Speeches*’ Tasnifu ya shahada za uzainifu,(haijachapishwa), Chuo Kikuu Cha Nairobi, Kuhenga C. (1977) *Tamathali za Usemi*.  Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.  Wamitila (2002) *uhakiki wa fasihi msingi na vipengele vyake*.  Nairobi Phoenix Publishers na  Mutiso(.1996) “Archaetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry;Kasida ya Burudai”.Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu:Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haujachapishwa).

Katika utafiti wetu pia tumeweza kuzungumzia kwa kina jinsi takriri na sitiari zilivyotumika katika *Utenzi wa Rasi’lGhuli* na ufanisi wake kwa ujumla.  Tulitimiza wajibu wetu kwa kujadili aina mbalimabli za sitiari kama vile sitiari kuu, sitiari chakavu, sitiari sahili, sitiari hisimseto, sitiari ya usuli, sitiari radidifu, sitiari ya kikaida na sitiari mseto.  Pia tumechanganua mbinu ya takriri na aina zake kama vile takriri irabu/vokali, takriri konsonanti, takriri neno/maneno na takriri silabi.  Hii ni ithibati tosha kuwa lengo hili tumelitimiza kikamilifu, ingawa tumejikita tu kwa aina ambazo zimejitokeza kwa wingi katika *Utenzi wa Rasi’lGhuli*.

## 5.2 Utathmini wa Nadharia Tete

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia tete mbili kuu ambazo ni::Utenzi wa Rasi'lGhuli una matumizi mengi ya takriri na sitiari yanayodhihirisha umbuji wa hali ya juu. Katika sura ya tatu na ya nne, tulithibitisha waziwazi kwamba, kupitia kwa matumizi mengi na mazuri ya takriri na sitiari, mtunzi aliweza kuonyesha ujuzi wake katika kuibua dhana tofauti za hali ya juu.

Tuliweza kuthibitisha ukweli wa nadharia hii tete kwa kuangazia jinsi vipengele vya fani vilivyoweza kuingiliana na kujengana. Pia tuliweza kuangazia jinsi *Utenzi wa Rasi'lGhuli* umesheheni matumizi mengi ya takriri na sitiari. Kupitia kwa mbinu hizi mbili tuleweza kuelezea kwa kina jinsi kazi ya mtunzi ilivyorahisishwa na kufanywa ya kuvutia na yenye mnato wa hali ya juu kwa wasomaji na wasikilizaji.Mbinu hizi mbili zimesheheni katika utenzi wote kutoka mwanzo hadi mwisho, hivyo kudhihirisha umuhimu wake katika kuendeleza hadithi pamoja na kufanikisha maudhui yake. Tumeweza kuthibitisha ukweli wa nadharia hii kwa kuangazia kwa kina katika sura ya tatu na ya nne. Kwa kweli matumizi ya mbinu hizi mbili za tamathali yaliweza kuchangia pakubwa katika kuendeleza msuko wa hadithi pamoja na kufanikisha maudhui yake. Kwa mfano, kupitia kwa matumizi ya sitiari, mtunzi alifanikiwa kuibua maudhui tofauti na kuifanya hadithi kuwa ya kuvutia na kupendeza. Vile vile matumizi mengi na mazuri ya takriri yaliweza kuipa kazi ya mtunzi sura ya kishairi na pia kuendeleza msuko wa hadithi kwa njia ya kupendeza.

Kwa hivyo kulingana na maoni yetu tuleweza kufanikiwa kuthibitisha nadharia tete ya pili. Hata hivyo kuna haja ya uchunguzi zaidi kufanywa ili kurahisisha uelewekaji wa *Utenzi wa Rasi'lGhuli.*

Kimsingi ni kwamba sitiari na takriri zinazojitokeza katika *Utenzi wa Rasi'lGhuli* ni bia na zina uamilifu mwingi wa kisanii. Vile vile ni kama kitovu cha fani na maudhui ya utenzi wenyewe

## 5.3 Mapendekezo ya utafiti

Tumehakiki takriri na sitiari katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani na tuna hakika kwamba tumetoa msingi imara kwa wasomaji na wahakiki wa *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Tungependa kuwarai watafiti wengine walio na nia ya kuuhakiki utenzi huu wachunguze vipengele vingine vya tamathali za usemi ili kuufanya utenzi huu kueleweka zaidi kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu lugha iliyotumiwa ni mchanganyiko wa lahaja tofauti kama vile kiarabu, kingozi, kimvita na vilevile msamiati wa kale.

Kupitia uhakiki wa tamathali hizi ambazo ni kama vile taswira, jazanda, taharuki, toni, tashibihi, taashira na kadhalika. *Utenzi wa Rasi'lGhuli* utakuwa rahisi kueleweka na kuvutia wasomi wengi. La sivyo, wasomi wengi chipukizi wataupuuza kwa sababu ya uchakavu wa lugha iliyotumiwa.

Kwa upande mwingine tunapendekeza maudhui na dhamira kuchunguzwa kwa undani. Pia ulinganishi unaweza kufanywa baina ya utenzi huu na tenzi zingine za kale au hata pia za Kiswahili.

Utenzi huu pia unaweza kuchunguzwa kwa kutumia nadharia tofauti mbali na ya umuundo ambayo tumetumia. Hata hivyo ni vyema kutambua kuwa, utafiti huu una wajibu mkubwa katika nyanja za fasihi. Na umetoa mchango mahsusi katika mwanya uliokuwepo wa uhakiki wa suala la jukumu la takriri na sitiari, katika kufanikisha kazi ya mtunzi kifani.

## MAREJELEO


Abdulazizi M.H. (1979). *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry*; Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Abrahams M.H. (1947) *Glossary of Literary Terms* : *Toleo la tatu,* New York : Holt, Reinehart and Winston Inc.

Allen J.W.T. (1971). *Tendi: Six examples of a Swahili Classical verse form with Translations and Notes.* London; Heimann

Arege, T.I.M (2012) Narration in Swahili narrative poetry: *An Analysis of Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Tasnifu ya PhD. University of Nairobi. Haujachapishwa

Barry (1916) A course in general linguistic.Cambridge ;Cambridge University Press.

Culler J. (1975:4-5) *Structuralist Poetics*. London: Routledge and Kegan Paul

Davidson, George W,(1985).ChambersConcise 20th Century Dictionary.

Dyer (1973) *Classic African Animals: The big five, New York*, Winchester Press.

Earlich,V (1969)Russian Formalism:3rd Edition:The Hague;Mounton & Co.N V. Publishers.

Fowler,Henry Watson (1952).The Concise Oxford Dictionary of Current English..

Faqihi, B.M. (1979) *Utenzi wa Rasi'lGhuli. Dar es Salaam*, Tanzania Publishing House Ltd

Fiumara G.C. (1995) *The Metaphoric Process : Connections between Language and Life*. London New York, Routeledge

Fryer na Perkins (1985) *The Harper Handbook to Literature*/Northrop Frye, Sheridan Baker, George Perkins ; with a chronology of literature and world events by Barbara M. Perkins

Habwe J. (1999) '*Discourse : Analysis of Swahili Political Speeches'* Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu, haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Harmon (1986) A handbook to literature, New York, Macmillan.

Harries (1962) *Swahili Poetry :* Oxford Claredom Press.

Hichens, W (1972) *Al –Inkishafi S.A Nasir*, Nairobi: Oxford University Press.

Holman, C.H. (1960) A Handbook to Literature, New York : Odyssey Press Inc.

Knappert J. (1967) *Traditional Swahili Poetry" An investigation into the concept of East African Islam as reflected in the Utenzi* Literature. Leiden: E.J. Brill

_______(1971) *Swahili Islamic Poetry*. Leiden E.J. Brill

_______(1979) *Four centuries of Swahili verse*. London: Heinemman Ltd.

Kezilabi, E. (1997:59) *Crative writing in Swahili: Makala ya Kongomano la Uandashi wa Kibunifu katika Lugha za Kiafrika*. SOAS, London

Kuhenga C. (1977) *Tamathali za usemi*, Dar es Salaam: Eat Africa. Literature Bureau.

Lambert, H.E. (1965) *Some initiation songs of the Southern Kenyan Coast*, Swahili 35/149-67.

Lugwiri P.L.O (2009) Sitiari,Taashira na Tashibiha katika uwasilishaji wa dhamira katika Utenzi wa Tambuka. *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili* (MA) katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi (haujachapishwa).

Mbatiah M. (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi Standard Textbooks Grop and Publishing

Mungai P.K. (2005) *Uhakiki linganishi wa kifani wa Tenzi mikidadi na Mayasa na Swifa ya Nguvumali, Tasnifu ya Uzamili,* Chuo Kikuu cha Nairobi, Haijachapishwa.

Murray P. (1978) *Literary Criticism*. Harlow Essex, Longman Group.

Myers na Simms (1978) The Longman Dictionary of Poetic Terms : London, Longman.

________(2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Publishers.

Olali, T (2004*) The Veneration of the Prophet: The Role of Kasida Hamziyya. During the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya*. Tasnifu ya PHD (haijachapishwa).

Scott A.F. (1983) *Current Literary Terms* : A Concise Dictionary, London, Macmillan

Simpson P. (2004) *Stylistics : A Resoruce book for Students* : London : Routledge

Trimingham (1962) *Islam in Ethiopia*, London : L. Francass

Tuki (2006) *English – Swahili Dictionar*y. Dar es Salaam

____(2010) *A Standard Swahili – English Dictionary*, Nairobi University Press.

___ (1981*) Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi : Oxford University Press

Wales K. (2001) A *Dictionary of Stylsicts* : Toleo la Pili, Harlow : Pearson Education

Wamitila (2002) *Uhakiki wa Fasihi Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi Phoenix Publishers

_______(2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi Focus Publishers.

_____ (2008) *Kanzi ya Fasihi Misingi ya uchanganuzi wa Fasihi,* Nairobi Videmua Publihsers Ltd.

Wamitila K.W. (2002) *Uhakiki wa fasihi: Msingi na vipengele vyake,* Naiorbi: Phoenix Publishers.

Wa Mutiso (1996) "*Archaetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai*". Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

________ (2003) *Analysis of Swahili Islamic Poetry. Five Swahili Epic four Swahili women*. (Mswada haujachapishwa).